# DHAMIRA ZA NYIMBO ZA MICHEZO YA WATOTO ZINAVYOSAIDIA KUJENGA UJASIRI NA TABIA NJEMA KATIKA JAMIIYA WAZANZIBARI

**ALI KHAMIS JUMA**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2024**

# ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa "***Dhamira za Nyimbo za Michezo ya Watoto Zinavyosaidia Kuwajenga Ujasiri na Tabia Njema katika Jamii ya Wazanzibari***" kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya masharti ya shahada ya (M.A Kiswahili - Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

____________________________

Dkt.Hadija Jilala

**(Msimamizi)**

____________________________

Tarehe

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kukaririwa kwa mbinu ya kielektroniki kama kunakili, kutoa kopi au kurudufu sehemu yoyote ya tasnifu hii bila ya idhini kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

## TAMKO

Mimi **Ali Khamis Juma,** ninatamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii ya utafiti iitwayo**"*Dhamira za Nyimbo za Michezo ya Watoto Zinavyosaidia Kuwajenga Ujasiri na Tabia Njema katika Jamii ya Wazanzibari*"** ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa popote pale kwa lengo la kutunukiwa shahada yoyote katika Chuo Kikuu chochote.

__________________________

Saini

## TABARUKU

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa watoto wangu wapendwa Farhat, Ruqayyah, Nihlah, Khamis, Naylah, Hajj na Issa kwao iwe chachu ya kujali elimu na kujifunza kwa bidii ili iwawezeshe kufikia mafanikio ya kitaaluma na kutegemea katika nyanja zote za maisha.

## SHUKURANI

Kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambayeameniruzuku uhai hadi leo, na kunipa nguvu katika kufanikisha kazi yangu hii. Mshikamano wa Mola na Nafsi yangu daima ndio ulioniwezesha kusoma, kufanya utafiti na kuweza kutoa kazi hii kwa mafanikio makubwa.

Aidha, shukurani za pekee ziende kwa msimamizi wangu, Dkt. Hadija Jilala, kwa kukubali kuwa msimamizi wangu. Yeye alikuwa kwangu ni mshauri, mwelekezaji na mwalimu aliyenikosoa kwa busara na hekima kubwa kila ilipobidi kukosolewa na kuelekezwa.Kwa hakika cha kumlipa sina, lakini sitoacha kumuombea dua kwa Mwenyezi Mungu ili amzidishie moyo wa upendo na ampe nguvu ili aweze kuendelea kuwa hazina kubwa yenye kutegemewa kwa manufaa ya sasa na baadaye.

Pia, ninapenda shukurani zangu za dhati ziende kwa kaka yangu Dkt.Hamad Khamis Juma kwa kunipa motisha, ushauri na kuniongoza kuifanya kazi hii kila ilipobidi. Bila shaka, mchango wake ni mkubwa sana kwani alikuwa pamoja na mimi katika shida na raha katika kuhakikisha kuwa kazi hii imekamilika.

Halikadhalika, ninatoa shukurani maalumu kwa walimu wangu walionifundisha kozi mbalimbali za Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania,Kituo cha Zanzibar. Miongonimwao ni Dkt. Salma Hamad, Dkt. Omar Maguo na Dkt. Zelda Elisfa kwa moyo wao na ufundishaji wao mzuri.Aidha, ninaushukuru uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania pamoja na wanafunzi wenzangu wa Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii kwa **ushirikiano** walionipa na kunihimiza kuikamilisha kazi yangu haraka iwezekanavyo.

Mwisho, nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo nitaacha kuwashukuru wazazi wangu, wake zangu wapenzi;Bi. Amina Hajj Juma na Bi. Fatma Issa Simai, pamoja na watoto wangu. Ninawashukuru kwa ustahamilivu walioonyesha muda wote niliokuwa nikiwakosesha haki walizostahili kutokana na harakati za kufanya utafiti na uandishi wa kazi hii. Nyote nawambieni Ahsanteni sana, na Mwenyezi Mungu akuondosheeni matatizo na awalipe wema.

## IKISIRI

Utafiti ulilenga kuchunguza dhamira za nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema katika jamii ya Wazanzibari. Utafiti ulikuwa na malengo mahususi matatu; mosi, kubainisha nyimbo za michezo ya watoto, mantiki na miktadha ya uimbaji katika jamii ya Wazanzibari. Pili, kuchambua dhamira za nyimbo teule za michezo ya watoto katika jamii ya Wazanzibari. Na tatu, kuonesha jinsi dhamira za nyimbo hizo zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema.Mbinu za ushuhudiaji, usaili na majadiliano zilitumika katika ukusanyaji wa data ambapo data hizo zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa maelezo. Nadharia za Uchambuzi Matini na Mwitikio wa Msomaji zilitumika kuongoza uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti huu. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwaUtafiti huu ulibainisha mantiki na miktadha ya uimbaji wa nyimbo za michezo ya watoto. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa kuna nyimbo mbalimbali za michezo ya watoto ambazo zina maana tofauti tofauti na huimbwa katika miktadha mbalimbali. Miongoni mwa nyimbo hizo ni Duara, Moja mbili tatu, Mpilipili, Panya, Maji ya moto, Nalia na A e i o u, Tuamkapo asubuhi, Kidabwada, Turukeruke, Unakwenda wapi, Ndege kumi porini na Watoto wazuri. Nyimbo nyingine ni Baba kasafiri, Kificho, Mnara wa baba, Kaskazi, Sukari ya Mahonda, Ndugu yetu na Twende sikukuu. Nyimbo hizo huimbwa katika miktadha ya shuleni, nyumbani na mitaani, wakati wa mchana, jioni na usiku wa mapema. Kuhusu dhamira za nyimbo, matokeo ya utafiti yanabainisha kwamba nyimbo za michezo zina dhamira mbalimbali kulingana na mahitaji ya jamii. Miongoni mwa dhamira hizo ni pamoja na kuwajenga watoto kiakili na kifikira, kuwafunda na kuwaendeleza katika maadili mema, kuwaburudisha na kuwastarehesha. Dhamira nyingine ni pamoja na kuwajengea watoto mioyo ya kizalendo, kutafuta elimu, kupanga malengo katika maisha, kuwafundisha kutamka maneno ya lugha, kuwafundisha kuhesabu na kuwajengea uwezo wa uvumbuzi. Pia, hulenga kuwasaidia watoto katika kuwakuza kimwili na kimaadili kulingana na jamii wanayoishi. Kuhusu jinsi nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa michezo ya watoto inawajenga ujasiri kwa huwakuza kiakili na kifikra, kufanyakazi kwa bidii, kuepuka utegemezi katika maisha, kutafuta elimu na kupanga malengo katika maisha yao ya kila siku. Kuhusu tabia njema, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa michezo huwakuza watoto kuwa na maadili mema, kuwa na moyo wa kizalendo, kuepuka kiburi, kufanya mazoezi ya viungo na kuwapenda wazazi. Kwa hakika dhamira hizo, huwajenga watoto kuwa na tabia njema katika jamii ambapo hufanya mambo yanayokubalika na kuacha mambo yote yasiyokubalika katika jamii yao. Mtafiti anapendekeza kwa wazazi na serikali kutilia maanani umuhimu wa nyimbo na michezo ya watoto kwa kujumuishwa katika mitaala ya elimu. Mwisho, mtafiti anapendekeza tafiti zaidi zifanyike kuchunguza umuhimu wa michezo ya watoto kwa jamii ya baadaye.

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| Bi | Bibi |
| Bw. | Bwana |
| Dkt | Daktari |
| MA | Masters of Arts |
| n.k | na kadhalika |
| Prof. | Profesa |
| TAKILUKI | Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| Uk. | Ukurasa |

# YALIYOMO

Ithibati ........................................................................................................ i

Hakimiliki ........................................................................................................ ii

Tamko ........................................................................................................ iii

Tabaruku ........................................................................................................ iv

Shukrani ........................................................................................................ v

Yaliyomo ........................................................................................................ ix

**SURA YA KWANZA ........................................................................................ 1**

**1.0 UTANGULIZI WA JUMLA ........................................................................ 1**

1.1 Utangulizi ........................................................................................ 1

1.2 Usuli wa Utafiti ........................................................................................ 1

1.3 Tatizo la Utafiti ........................................................................................ 3

1.4 Malengo ya Utafiti ........................................................................................ 3

1.4.1 Lengo Kuu ........................................................................................ 4

1.4.2 Malengo Mahususi ........................................................................................ 4

1.5 Maswali ya Utafiti ........................................................................................ 4

1.6 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................................ 4

1.7 Upeo wa Utafiti ........................................................................................ 5

1.8 Mpangilio wa Tasnifu ........................................................................................ 6

1.9 Muhutasari wa Sura ya Kwanza ........................................................................ 7

**SURA YA PILI ........................................................................................ 8**

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA NADHARIA ........................................ 8**

2.1 Utangulizi ........................................................................................ 8

2.2 Maandiko kuhusu Nyimbo ........ 8

2.2.1 Maana ya Nyimbo ........ 8

2.2.2 Chimbuko la Nyimbo ........ 10

2.2.2 Uainishaji wa Nyimbo ........ 11

2.2.3 Kazi Tangulizi kuhusu Nyimbo ........ 12

2.2.4 Nyimbo za Michezo ya Watoto ........ 12

2.2.5 Fani na Maudhui katika Nyimbo ........ 14

2.3 Nadharia za Utafiti ........ 18

2.3.1 Nadharia ya Uchambuzi wa Matini ........ 18

2.3.2 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ........ 20

2.4 Muhutasari wa Sura ya Pili ........ 21

**SURA YA TATU ........ 22**

**3.0 MBINU ZA UTAFITI ........ 22**

3.1 Utangulizi ........ 22

3.2 Mkabala wa Utafiti ........ 22

3.3 Aina ya Utafiti ........ 22

3.4 Eneo la Utafiti ........ 23

3.5 Sampuli na Usampulishaji ........ 23

3.5.1 Sampuli ........ 24

3.5.2 Usampulishaji ........ 24

3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........ 26

3.6.1 Mbinu ya Ushuhudiaji ........ 26

3.6.2 Mbinu ya Usaili ........ 26

3.6.2 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi ........ 27

3.7 Uchanganuzi wa data ..... 27
3.8 Uthabiti na ukubalifu wa data ..... 28
3.8.1 Uthabiti na Ukubalifu wa Data ..... 28
3.8.2 Kukubalika kwa Data za Utafiti ..... 28
3.9 Vifaa vya Utafiti ..... 29
3.10 Itikeli ya Utafiti ..... 29
3.11 Muhutasari wa Sura ya Tatu ..... 29
**SURA YA NNE ..... 31**
**4.0 UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA ..... 31**
4.1 Utangulizi ..... 31
4.2 Taarifa za Wahojiwa ..... 31
4.2.1 Jinsia ya Wahojiwa ..... 31
4.2.2 Umri wa Wahojiwa ..... 31
4.2.3 Elimu ya Wahojiwa ..... 32
4.3 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data ..... 32
4.3.1 Nyimbo za Michezo ya Watoto, Mantiki na Miktadha ya Uimbaji ..... 33
4.3.2 Dhamira za Nyimbo za Michezo ya Watoto ..... 49
4.3.3 Dhamira za Nyimbo Zinavyosaidia Kujenga Ujasiri na Tabia Njema ..... 56
4.3.3.2 Kuwajenga Ujasiri kwa Kufanya Kazi kwa Bidii ..... 58
4.3.3.3 Kuwajenga Ujasiri kwa Kuepuka Utegemezi katika Maisha ..... 58
4.3.3.4 Kuwajenga Ujasiri wa Kutafuta Elimu ..... 59
4.3.3.5 Kuwajenga Ujasiri wa Kupanga Malengo katika Maisha ..... 60
4.3.4 Kuwajenga Tabia Njema ..... 61
4.3.4.1 Kuwajenga Tabia ya kuwa na Maadili Mema ..... 62

4.4 Muhutasari wa Mjadala wa Matokeo ya Utafiti ........................................... 69

4.5 Muhutasari ........................................................................................... 69

**SURA YA TANO ........................................................................................... 71**

**5.0 MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................................. 71**

5.1 Utangulizi ............................................................................................. 71

5.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti ........................................................ 71

5.2.3 Nyimbo za Michezo ya Watoto, Mantiki na Miktadha ya Uimbaji ............... 72

5.2.2 Dhamira za Nyimbo za Michezo ya Watoto ............................................... 73

5.2.3 Nyimbo za Michezo ya Watoto Zinavyowajenga Ujasiri na Tabia Njema.... 73

5.3 Hitimisho .............................................................................................. 74

5.4 Mapendekezo ya Utafiti ........................................................................ 75

**MAREJELEO ................................................................................................. 77**

**Maswali ya Mwongozo wa Mahojiano ......................................................... 82**

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu umechunguza dhamira za nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema katika jamii ya Wazanzibari. Vipengele vya msingi vilivyoangaziwa katika sura hii ni usuli wa utafiti, tatizo ta utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vyengine ni umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti na muundo wa tasnifu.

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Wataalamu mbalimbali wanaeleza kuwa nyimbo za michezo ya watoto ni utanzu muhimu katika fasihi simulizi ambao hutumiwa katika jamii na kabila mbalimbali. Miongoni mwa wataalamu hao ni Beja (2001), Timamy (2002), Wamitila (2003) na Mulokozi (2017). Kwa mujibu wa Mulokozi (2017) anatoa maana ya nyimbo kwa namna inavyowasilishwa kwa kusema kuwa nyimbo ni kila kinachoimbwa. Hivyo, nyimbo za michezo ya watoto ni zile ambazo huimbwa na watoto wanapokuwa katika michezo yao ya kawaida nyumbani, mitaani na hata shuleni.

Katika uimbaji wa nyimbo za michezo ya watoto huwapo pande mbili ambazo ni fanani yaani mwimbaji au mwongozaji na hadhira yaani watoto wanaosaidia kuimba au wanaoitikia (Wamitila, 2003). Kitu cha msingi na kuzingatia ni kuwa watoto wanaoimba nyimbo huwa na umri tofauti ambapo mara nyingi kuanzia miaka minne hadi kumi na mbili. Hata hivyo, nyimbo hizo huwasilisha ujumbe tofauti na wenye viwango tofauti vya uelewa kwa watoto wanaoimba. Hivyo, bila shaka fanani huyo

huweza kuwa na lengo la kufikisha ujumbe wake nje ya mipaka ya hadhira ya msingi. Kwa hivyo, nyimbo za michezo ya watoto huwa ni msingi unaomchochea mwimbaji (yaani, mtoto); kufikisha ujumbe katika jamii. Mbali na dhima kuu mtoto, huwasilisha ujumbe kwenda kwa hadhira pana zaidi ya mtoto. Kwa hiyo, inaaminika kuwa nyimbo za michezo ya watoto hujenga daraja la kifalsafa kati ya mama au mlezi, mtoto na jamii.

Kwa kawaida, nyimbo hizo huimbwa kwa kuzingatia sifa za utendekaji wa fasihi ya watoto. Miongoni mwasifa hizo ni sentensi fupi fupi na lugha nyepesi (Bakize, 2014). Uimbaji wa wa nyimbo za michezo ya watoto huenda sambamba na matendo kama vile kupiganapigana au kuchezacheza pamoja huku wakishirikiana.

Kwa hivyo, uimbaji wa nyimbo na vitendo wanavyofanya watoto katika michezo yao huwa na uhalisia fulani katika unaoakisi maisha yao ya kila siku hapo baadaye. Kulingana na hali hiyo, mtafiti aliona kwamba nyimbo za michezo ya watoto katika jamii ya Wazanzibari, kama zilivyo tanzu au vipera vyengine vya nyimbo, hubeba dhamira zenye ujumbe kwa jamii. Watoto katika jamii ya Wazanzibari huendesha maisha yao ya kila siku katika nyanja mbalimbali za maisha ikiwamo utamaduni na sanaa. Kupitia mafunzo yatokanayo na nyimbo za watoto hujengeka kiujasiri na tabia njema.

Aidha, mtafiti anaelewa kuwa kuna baadhi ya tafiti zimeshafanywa kuchunguza dhamira zinazojitokeza katika nyimbo mbalimbali za watoto, lakini tafiti hizo hazijashughulikia jinsi dhamira hizo zinavyosaidia kuwajenga watoto ujasiri na tabia njema katika jamii. Kwa kuzingatia hilo, mtafiti alichunguza dhamira za nyimbo za

michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema katika jamii. Pamoja na mambo mengine, utafiti huu ulichunguza dhamira zinazojitokeza katika nyimbo teule na kuonesha jinsi nyimbo hizo zinavyowajenga watoto kuwa majasiri na wenye tabia njema katika jamii yao.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Katika jamii nyingi za Waswahili, nyimbo za michezo ya watoto huimbwa wakati wanapokuwa wamekusanyika pamoja nyumbani au mtaani nyakati za jioni na usiku wa mapema wakiwa wamesharudi shuleni na madrasa. Pia, wakiwa shuleni hutumia nyimbo za michezo ya watoto katika baadhi ya masomo yao na shughuli za kila siku za maisha.Watafiti mbalimbali wamechunguza nyimbo katika michezo ya watoto wakiwamo Mbarouk (1994) na Nassor (2016). Kwa ujumla, watafiti hao wametafiti mambo ya msingi ambayo mtafiti yana mchango katika utafiti huu.Pamoja na mchango wa tafiti hizo, mpaka hivi sasa hakuna utafiti uliojielekeza kuchunguza dhamira za nyimbo za michezo ya watoto zinavyowajenga ujasiri na tabia njema. Hali hiyo inatoa pengo la maarifa kwa sababu tunashindwa kujua dhamira hizo zinawasaidiaje watoto katika maisha yao ya baadaye. Katika kuliziba pengo hilo, mtafiti aliona kuwa ipo haja ya kutafiti dhamira hii katika nyimbo za michezo ya watoto ili kuonesha jinsi dhamira za nyimbo hizo zinavyosaidia kuwajenga watoto ujasiri na tabia njema.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu moja na malengo mahsusi matatu kama ifuatavyo:

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwakuchunguza dhamira za nyimbo za michezo ya watotozinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema katika jamii ya Wazanzibari.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahasusi yafuatayo:

(i) Kubainisha nyimbo za michezo ya watoto, mantiki na miktadhaya uimbaji katika jamii ya Wazanzibari.

(ii) Kuchambua dhamira za nyimbo teule za michezo ya watoto katika jamii ya Wazanzibari.

(iii) Kuonesha jinsi dhamira za nyimbo hizo zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Ili kufanikisha malengo mahususi, utafiti huu uliongozwa na maswaliyafuatayo:

(i) Kuna nyimbo zipi za michezo ya watoto, zina maana zipi na zinaimbwamiktadha ipi katika jamii ya Wazanzibari?

(ii) Ni dhamira zipi za nyimbo teule za michezo ya watoto katika jamii ya Wazanzibari?

(iii) Ni kwa jinsi gani nyimbo za michezo ya watotohusaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unatarajiwa kuwa na umuhimu kama ifuatavyo:

Kwanza, utafiti huu utatoa mchango mkubwa katika uwanja wa fasihi hasa kwenye utanzu wa nyimbo hususankatika kipera cha nyimbo za michezo ya watoto. Wasomi na watafiti kujua umuhimu wa nyimbo katika michezo ya watoto na kuelewa jinsi nyimbo hizo zinavyowaanda kwa ajili ya maisha ya baadaye.

Pili, utafiti huu utakuwa ni nyenzo ya kuwashajihisha wazazi kuwaruhusu watoto kushiriki katika michezo yao ya asili ya kila siku. Jamii itapata kujua jinsi nyimbo za michezo ya watoto zinavyoibua dhamira mbalimbali zinazowajenga ujasiri na tabia njema katika maisha yao ya baadaye.

Tatu, utafiti huu utatoa mwanga kwa jamii katika kutilia maanani manufaa ya nyimbo zawatoto katika kuwajenga ujasiri na tabia njema. Wazazi na jamii kwa ujumla watawahamasisha watoto wao kuimba na kucheza michezo mbalimbali ya asili. Hivyo, watawapunguzia majukumu ili kufika wakati wa kucheza waweze kushiriki katika michezo hiyo.

Nne, utafiti huu utaamsha hamasa na ari kwa watunga mitalaa kuona haja ya kuingiza michezo ya watoto katika elimu ya maandalizi,msingi hata sekondari. Matokeo ya utafiti huu yataonesha jinsi nyimbo na michezo ya watoto inavyowajenga watoto kimwili na kimaadili. Hivyo, kuona umuhimu wa kuendeleza na kukuza nyimbo na michezo ya watoto

## 1.7 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza dhamira za nyimbo za watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema katika jamii ya Wazanzibari. Kwa kuwa jamii ya Wazanzibari ni kubwa, utafiti huu utajikita katika Mkoa wa Kaskazini Unguja ambapo data

zitakusanywa katika vijiji vya Mahonda, Kinduni na Donge Mtambile.Pia,utafiti uliteua nyimbo maalumu ambapo katika nyimbo hizo, mtafiti alichambua dhamira na kuonesha jinsi zinavyosaidia kuwajenga watoto ujasiri na tabia njema. Kupitia vipengele hivi mtafiti alipata kujua kwa marefu na mapana mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za michezo ya watoto, ambapo Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, Uchambuzi Matini naMwingiliano Matini zilimuongoza mtafiti katika uwasilishaji na uchanganuzi wa data.

## 1.8 Mpangilio wa Tasnifu

Baada ya utafiti huu kukamilika, ripoti yake imeandikwa kwa muundo wa tasnifu. Tasnifu hii imegawanyika katika sura tano ambapo sura ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla ambao unajadili vipengele kama vile usuli wa utafiti, tatizo la utafiti na malengo ya utafiti. Vilevile, maswali ya utafiti na umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi ambapo inaonesha mapitio ya kazi tangulizi mbalimbali zilizofanywa na wataalamu kuhusiana na nyimbo za michezo ya watoto. Sura hiyo pia inabainisha na kujadili nadharia zilizotumika katika uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti huu na jinsi ilivyoongoza uchambuzi huo. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti na eneo la utafiti ambapo sura hii inaanza kwa kutoa ufafanuzi kuhusu usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji wa data. Pia,vipengele vya uhalali na uimara wa zana za utafiti, mbinu za uchambuzi wa data na uzingativu wa itikeli ya utafiti vimebainishwa na kujadiliwa katika sura hii. Sura ya nne inahusu uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa data na mjadala wa matokeo ya

utafiti. Sura ya tano ambayo ndio ya mwisho inatoa muhutasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo kwa tafiti zijazo.

## 1.9 Muhutasari wa Sura ya Kwanza

Katika sura hii mtafiti amebainisha na kujadili vipengele vya msingi vinavyozingatiwa katika utafiti wa kitaaluma. Vipengele vya msingi vilivyoangaziwa katika sura hii ni pamoja na usuli wa mada ya utafiti, tatizo ta utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhumu wa utafiti, upeo wa utafiti na muundo wa tasnifu.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia kazi tangulizi mbalimbali zinazohusiana na mada pamoja na dhana muhimu zilizotumika katika utafiti huu. Mambo yanayojadiliwa nidhana ya nyimbo, maana na aina za nyimbo. Umuhimu wa nyimbo kwa jamii, dhanaya nyimbo za michezo ya watoto. Kwa kumalizia sehemu hii inahitimishwa kwa kiunzi cha nadharia kinachotumika katika tasnifu hii.

## 2.2 Maandiko kuhusu Nyimbo

Katika sehemu hii mtafiti anafafanua na kujadili chimbuko la nyimbo, maana ya nyimbo na aina za nyimbo. Pia, anachambua kazi tangulizi kuhusu nyimbo za michezo ya watoto, vipengele vya fani na maudhui katika nyimbo za michezo ya watoto.

### 2.2.1 Maana ya Nyimbo

Wataalamu mbalimbali wa fasihi wamejaribu kufasili maana ya nyimbo. Miongoni mwa wataalamu hao ni Mazigwa (1991) ambaye anafasili nyimbo kuwa ni kifungu cha maneno yaliopangwa katika utaratibu maalumu wenye kutekeleza mapigo ya muziki. Kawaida, wimbo huwa hutumia lugha ya mkato ambayo hufuata mapigo ya ala za muziki kwa mfano ngoma, zeze, marimba, njuga, filimbi nakadhalika. Nyimbo pia huenda sambamba na ngoma kwani wakati wa kuimba ngoma huendelea kulia na wakati huo huo waimbaji hucheza. Aidha, wengine huimba kwanza, halafu ngoma kufuatia na wachezaji hufuata mlio wa ngoma.

Nkwera na wenzake (1992), wanafasili wimbo kuwa ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Katika kufafanua maana ya muziki wanaeleza kuwa ni mpangilio wa sauti za ala na uimbaji unaoleta athari fulani kwa binadamu kupitia hisia na akili yake. Nkwera na wenzake wanahitimisha kwa kueleza kuwa jambo muhimu katika nyimbo ni uimbaji, sauti za ala lakini miondoko sio lazima.

Haji na wenzake (2004:4) wamefasili nyimbo kuwa ni mashairi mafupi ambayo hujitokeza katika sehemu nyingi za jamii. Wanaendelea kufafanua nyimbo huwa ni fupi aghlabu huwa ni ubeti mmoja tu wenye mistari mitatu. Nyimbo huweza kuambatana na sanaa ya kughani, ngoma, makofi au muziki. Aidha, nyimbo huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi ambayo hupangwa kwa utaratibu au **muwala** wenyemapigo ya kimziki au mizani.

King´ei na Kisovi (2005) pia wamefasili nyimbo kuwa ni utungo wenye mpangilio maalum wa maneno wenye mahadhi ambao huambatana na shughuli au jambo fulani.Katika wimbo, sauti ya muimbaji au waimbaji huwatia moyo watu kama vile wavuvi au wakulima katika kazi zao. Mara nyingi, nyimbo huimbwa kwa burudani katika sherehe kama vile harusi, ibada za kidini, kafara, matambiko, jando na unyago.

Mulokozi (1996) amefasili wimbo kuwa ni kila kinachoimbwa, hivyo ni dhana inayojumuisha tanzu nyingi kama vile hadithi huweza kuingia katika utanzu huu pindi zinapoimbwa. Anaendelea kueleza kuwa vitu muhimu vya kutambulisha nyimbo ni kama vile, muziki, sauti ya muimbaji, muziki wa ala, matini au maneno yanayoimbwa, hadhira inayoimbiwa na muktadha unaofungamana na wimbo huo.

Kutokana na fasili za wataalamu mbalimbali imedhihirika kuwa nyimbo zina sifa maalumu za kuzitambulisha. Miongoni mwa sifa hizo ni maneno yanayoimbwa na yenye mpangilio maalumu, hufungamana na muktadha, sauti ya muimbaji au waimbaji. Aidha, imebainika kuwa nyimbo katika jamii zina dhima mbalimbali, kama vile kutumbuiza na kumpa msikilizaji au muimbaji mwenyewe burudani. Pia, hutumiwa kuwahamasisha watu kufanya jambo fulani kwa kuchochea hisia za kuchangamkia shughuli inayofanyika; kwa mfano kuburura magogo, kutwanga au kulima. Sambamba na hayo, nyimbo hutumika kurithisha utamaduni wa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa hivyo, nyimbo zinaweza kutumika kuhifadhi historia ya jamii kutoka kizazi hadi kizazi, kwa mfano, matokeo kama ya vita. Kwa muhutasari, tunaweza kueleza kuwa nyimbo ni njia nzuri ya kuelimisha na kupitisha maarifa mbalimbali miongoni mwa wanajamii.

### 2.2.2 Chimbuko la Nyimbo

Msokile (1992: 46) anaeleza kuwa nyimbo zinazobuniwa kimsingi hazitofautiani naushairi katika fasihi, ndio maana ameweka nyimbo pamoja na ushairi. Haji na wenzake(1992: 36) wanaeleza kuwa nyimbo ni utanzu wa ushairi, na kwamba tanzu zakenyengine ni tenzi. Maana hiyo inaungwa mkono na Hamad (2008:40) kuwa nyimbo zinatokana na ushairi simulizi.Anaendelea kufafanua kuwa nyimbo ni utanzu mkongwe wa fasihi simulizi ambao ulianza kuimbwa kwa mahadhi ya sauti tu. Katika siku za baadaye ikaongezeka kupiga kofi ili kukoleza mahadhi hayo nahata kwa kutumia ala mbalimbali zinazokoleza muziki wa nyimbo hizo.

Wataalamu mbalimbali wanaeleza kuwa ni vigumu kupata chanzo halisi cha nyimbo za watoto (taz. Mulokozi, 1975; Iona na wenzake, 1997; Cuddon, 1998). Hata hivyo,

nyimbo hizi zimekuwepo katika jamii kwa muda mrefu sana kama sehemu ya fasihi simulizi ya jadi. Kwa kuwa fasihi simulizi ni utanzu hai (Mulokozi, 1996; Samwel 2012), nyimbo za watoto kama utanzu wa fasihi simulizi zimekuwa zikizaliwa, kukua na hata kufa. Pamoja na nyimbo hizi kuitwa za watoto, baadhi yake zimekuwa zikiimbwa na hata watu wazima kutokana na umuhimu wake kwa jamii.

### 2.2.2 Uainishaji waNyimbo

Okupweho (1992:1227) anaeleza kuwa katika jamii watu hutumia vigezo tofauti tofauti vya kuainisha nyimbo na maghani. Vigezo hivyo ni kama vile maudhui,dhamira, ala zitumikazo, mitindo ya uimbaji, miktadha na muimbaji wa nyimbohizo.Mtaalamu huyo, alipendekeza kitumikekigezo cha maudhui katika kugawa ushairi waKiafrika kwa kubainisha dhamira kuu za ushairi huo.Uanishaji huo unaungwa mkono na wanafasihi wengine kama vile; Finnegan (1970), Mulokozi (1989 na 1996), Mazigwa (1991), Nkwera nawenzake (1992), Msokile (1992), Wamitila (2005) na Kingei na Kisovi (2005).

Kupitia kigezo hicho cha uainishaji wa nyimbo, tunapata nyimbo za aina mbalimbali kama vilenyimbo za dini, nyimbo za harusi, nyimbo za **sifo**, nyimbo za watoto na nyimbo zataarabu. Hata hivyo, uanishaji wa nyimbo umekuwa na utata kwa sababu hakuna kigezo maalumu kinachotumika katika uainishaji wake. Hii inatokana na maelezo ya Wamitila (2002) anapoeleza kuwa kuna aina nyingi za nyimbo ambapo hutofautiana kwa aina hizo katiya wataalamu mbalimbali. Vilevile, tatizo la kuwa na nyimbo za aina Fulani zilizoainishwa na mtaalamu mmoja na mtaalamu mwengine huainisha aina nyingine za nyimbo.

Katika wataalamu wa fasihi tuliowabainisha hapo juu ni wanafasihi wachache waliofafanua nyimbo za watoto. Miongoni mwa wanafasihi hao waliobainisha nyimbo za michezo ya watoto ni Mulokozi (2006) na Haji na wenzake (1983).

### 2.2.3 Kazi Tangulizi kuhusu Nyimbo

Utanzu wa nyimbo umebahatika kutafitiwa katika vipengele vyake muhimu vya fanina maudhui, kama vile dhamira, matumizi ya lugha, tafsida, ishara na picha. Kwa mfano, nyimbo za kilimo za kabila la Wafipa zimeangaliwa fani, maudhui, nadhima yake. Nyimbo za harusi za kabila la Wapagwa zimefanyiwa utafiti katika matumizi ya lugha, dhima na dhamira zilizomo. Nyimbo za waimbaji walemavu zimetafitiwa dhamira zake mfano nyimbo zinazohusu UKIMWI zimefanyiwa utafitikwa kuangaliwa lugha yake kisanii na namna inavyoibua maudhui yanayohusu ugonjwa huo. Utafiti pia umefanywa katika nyimbo za jando na unyago za jamii yaWamwera na kuangalia mfungamano wake na jamii hiyo.

Kwa mujibu wa tafiti mbalimbali zilizofanyika kuhusu utanzu wa nyimbo nakugusia nyimbo za harusi, jando na unyago na nyimbo za taarabu. Kupitia tafiti hizo mtafiti amebaini kuwa nyimbo za michezo ya watoto hazijashughulikiwa ipasavyo. Hivyo, amepata hamasa ya kufanya utafiti wa nyimbo za michezo ya watoto kama ni aina moja yanyimbo zilizokuwa hazijatafitiwa sana.

### 2.2.4 Nyimbo za Michezo ya Watoto

Ameir (1983) amezungumzia suala la aina ya nyimbo za michezo yawatoto, kuwa lugha yake inayotumika huwa ni nzito, yenye mafumbo na picha,hivyo huwa nzito kuhakiki ujumbe uliomo kwenye nyimbo hizo ama michezo hiyona wazee.

Anaendelea kwa kusema, kawaida katika sehemu nyingi za nchi yetu,watu hula chajio, baada ya watu kusali sala ya Isha. Kwa watoto wadogo ambaokutwa huwemo katika pirika mbalimbali, ikikaribia wakati huu, huwa taabani kutokana na machofu. Wakishakoga ili wabaki macho na waweze kula chakula hicho, hufanyika kitu cha kuwafanya wawe macho hujikuta wakicheza michezo mbalimbali ambayo ndani yake huwemo nyimbo zenye maana.

Aidha, ameongezea kwa kusema kuwa nyimbo nyingi za michezo ya watoto huwa hazina mantiki, yaani mpangilio wa vina na mizani, na hivyo huonekana hazina maana. Ukosefu huu wa mantiki kwenye nyimbo za michezo ya watoto, ndiyo husababisha jamii kutozitilia maanani sana na kuona hazina mchango mkubwa katikamakuzi ya watoto wenyewe kimaadili. Ameir (1983) ameelezakuwa katika kisiwa cha Pemba imo michezo mingi tu ya watoto, tatizo ni kwamba wanajamii huchukulia nyimbo zilizomo michezoni kuwa hazina maana, huimbwa ziendane na mshindo na mpangilio mzima wa mchezo na hivyo, huonekana kuwadhima yake kubwa ni kuburudisha tu. Anafafanua kwa kusema kuwa, ukosefu huu wa mantiki ndani ya nyimbo hizi, ndio wanajamii hawazitilii maanani sana na kuona hazina mchango mkubwa katika makuzi ya watoto wenyewe kimaadili. Lakini ukweli ni kwamba, nyimbo zamichezo ya watoto ukizichunguza kwa ndani zina taathira kubwa kwa wanajamii.Hivyo, kazi ya wataalamu hawa ina mchango katika utafiti huu, hata hivyo haijashughulikia dhamira za nyimbo za watoto zinavyowajenga ujasiri na tabia njema.

Naye, Ali (1969:20) alichunguza nyimbo za michezo ya watoto ili kuibuafani na maudhui katika hizo. Kupitia utafiti wake anaeleza kuwa nyimbo za kuburudisha

watoto katika michezo yao huonekana kutoka kilakabila. Anaendelea kueleza kuwa maudhui mengi ya nyimbo hizo, mara nyingi humuhusu mtoto na hali yake katika jamii au mtoto na uhusiano wake na mama.Kwa upande mwengine, nyimbo nyingi za michezo ya watoto, huwashinda wahakikiwa maudhui kutokana na lugha yake. Lugha yenyewe huwa nzito, yenye picha, na mafumbo.Hivyo, wahakiki wengi wanakuwa na shaka kwa kudhani kuwa huenda watoto wakawa wametungiwa nyimbo hizi na wakubwa. Aidha mtaalamu huyu anafafanua kwa kusema kuwa, nyimbo za michezo ya watoto zitakuwa hazikutendewa haki iwapo hazitoangaliwa vipengele vyote vya kisanaa.

### 2.2.5 Fani na Maudhui katika Nyimbo

Mulokozi na Kahigi (1979: 54) wamefasili kuwa fani kama sanaa na ni jumla ya vipengele vya lugha vilivyowekwa katika mpangilio mahususi ili kutoa maana fulani. Vipengele vya lugha kwa sababu lugha ndio nyenzo kuu ya kuimba kazi ya Sanaa na kufikisha ujumbe wa mawazo yanayozungumziwa.

Mulokozi (1975) katika kazi yake iitwayo fasihi ya Kiswahili anaeleza kuwa ingawa nyimbo zinazoimbwa na watoto kwa ajili ya kujifurahisha, zinabeba ujumbe muhimu katika kuyaongoza mawazo na fikira zao katika masuala muhimu yanayohusu jamii yao. Anaendelea kufafanua kuwa ni vigumu kuelewa asili ya kila wimbo kwa sababu kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi simulizi, nyimbo za watoto huibuka na hubadilika kulingana na wakati na mazingira.

Naye Ndulute (1977) anafafanua nyimbo za watoto huwa ni zile nyimbo zinazoimbwa na watoto wakiwa shuleni au katika michezo yao ya kila siku.

Anendelea kueleza kuwa watoto wanapokuwa katika michezo hiyo huimba nyimbo ambazo huzikumbuka hata wanapokuwa watu wazima. Katika kazi yake anafafanuwa kuwa nyimbo za watoto huakisi shughuli mbalimbali zinazofanywa na jamii iliyowazunguka.

Mbarouk (1981) alichunguza nyimbo za michezo ya watoto na kubaini kuwa nyimbo za watoto ni burudani kwa watoto na hutumia lugha rahisi yenye kueleweka na kawaida ni lugha isiyokuwa na tamathali za semi. Mbarouk anaweka msisitizo kwamba nyimbo hizi ziimbwe kwa kuzingatia matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kwa hakika, Mbarouk alishitushwa na matumizi makubwa ya lugha ya Kiingereza katika nyimbo za Kiswahili na kasumba kwamba kujua Kiingereza ndio kustaarabika. Mbarouk anaibuka na mawazo kwamba mafunzo na ujumbe uliomo katika nyimbo hizo huwafikia watoto kwa haraka zaidi kwa kutumia lugha yao waliyoimiliki. Mawazo ya Mbarouk (1981) yanakaziwa na Rwilomba (1994) aliyetafiti matumizi ya sanaa za maonesho kama njia ya kufundishia masomo ya Hisabati na Kiingereza katika shule za awali na msingi. Rwilomba aligundua kwamba nyimbo za watoto za Kiswahili zina mchango mkubwa katika kutolea maarifa ya masomo mengine kwa watoto. Hivyo, nyimbo za watoto husaidia kufundishia na kujifunzia kwa watoto.

Vilevile, Balisidya (1987) ameziangalia nyimbo za watoto za Kiswahili kwa kukubali kuwepo kwa nyimbo hizo katika jamii. Katika kazi yake, Balisidya anasema kuwa nyimbo za watoto zimekuwepo katika jamii mbalimbali tangu zamani. Nyimbo hizo zimekuwa zikiimbwa na kupokezana kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mawazo haya yanalingana na Mulokozi (1975) ila yanatusaidia kubaini kwamba nyimbo za watoto zinarithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Pia, yanashadidia kwamba

jamii ikibadilika basi na hata nyimbo za watoto katika jamii hiyo nazo zinabadilika. Hoja hii itatusaidia katika kujadili mabadiliko ya nyimbo za watoto za Kiswahili kiutendaji katika kipindi hiki cha sasa.

Msokile (1992) anafafanua kwamba kwa kawaida nyimbo za watoto za Kiswahili huongelea mazingira wanayoishi na kucheza watoto na kwamba zina dhima kubwa. Hapa Msokile anasisitiza kuwa kusambazwa kwa nyimbo hizo kutoka kizazi kimoja hadi kingine kuna sababisha mabadiliko ya nyimbo sambamba na mabadiliko ya kijamii. Hata hivyo, Msokile anatahadharisha kwamba wakati mwingine nyimbo hizi hazina maana kabisa lakini huimbwa tu ili kuiburudisha hadhira yake. Pia, anasisitiza kwambanyimbo hizi ni muhimu sana katika jamii kwa sababu zinaelimisha, kuburudisha, kuhuzunisha na zinaweka wazi mambo mbalimbali katika jamii.

Kayoka (1994) anaunga mkono mawazo ya Mbarouk (1981) kuhusu uwezo wa nyimbo za watoto katika kurahisisha ujifunzaji na ufundishaji wa masomo kwa watoto. Anatolea mfano wa jinsi nyimbo hizo zinavyoweza kutumika katika ufundishaji wa dhana za kibaolojia katika shule za msingi. Kayoka anaongezea faida nyingine kuwa, hupunguza utawala wa mwalimu darasani na kutoa uhuru kwa wanafunzi kujifunza zaidi kwa kutumia vionjo mbalimbali vya milango ya fahamu.

Senkoro (1996) alichunguza nyimbo jinsi zinavyoakisi masuala ya kijinsia na uhalisi wa maisha ya watoto katika jamii. Anaeleza kuwa nyimbo hizi hutumiwa kueleza mitazamo kuhusu ulimwengu, ndoa na waume. Pia, huelezea hofu, malalamiko, uchungu, hasira na matumaini yao. Anasisitiza kuwa katika jamii za mfumo jike kama zile za Wakaguru nyimbo hizi zinaonesha umuhimu wa kijamii kwa watoto wa kike kama viumbe huru wanaoshirikiana katika shughuli za kijamii, kiuchumi na

kiutamaduni. Senkoro anaendelea kusema kuwa nyimbo za watoto kutoka pwani ya Afrika ya Mashariki, ambapo mfumo wa kikabaila na dume umejikita, zinaonesha picha ya utumwa, umaskini na ukosaji wa haki za kijamii.

Omari (2008) amechunguza nyimbo za watoto kwa kutilia mkazo namna watoto wanavyochorwa na kushirikishwa kimajukumu katika muktadha wa kumjenga mtoto kiakili na kimatendo. Katika uchambuzi wake huo anatuangazia kwamba kuna haja ya kuzisikiliza nyimbo hizi kwa kuwa, mbali na kutoa burudani, hubeba ujumbe unaohitaji kuchambuliwa kitaalamu. Mawazo yake yanatusukuma kuzichambua baadhi ya nyimbo za watoto za Kiswahili na kubainisha jinsi zinavyopitisha ujumbe muruwa kwa jamii zinazozisikia nyimbo hizo. Tutayaendeleza mawazo ya Omari kwa kujikita katika kuchanganua utendaji na mustakabali wa nyimbo hizo katika mfumo wa teknolojia ya kidijiti. Hii inatokana na ukweli kwamba mfumo huu ndio unaoongoza katika kuyateka, kuyajenga na hata kuyabomoa mawazo na matendo ya watoto ulimwenguni kote.

Senkoro (2011) anafasili fani kuwa ni ujumla ya ufundi wakisanaa anaoutumia msanii katika kazi yake. Na maudhui ni yale yapatikanayo kutokana na mawazo, mafunzo na ujumbe uliomo katika kiini cha fani. Hivyo fasili hizi zitamsaidia mtafiti kuweza kuchambua kazi yake kwa umakini kabisa kwa kuangalia uwiano uliopo katika vipengele vya maudhui katika ya nyimbo za michezo ya watoto.

Kupitia kazi tangulizi zilizobainishwa hapo juu, mtafiti ameona na mawazo ya wataalamu na watafiti mbalimbali yanayodhihirisha nyimbo za michezo ya watoto. Kwa ujumla, nyimbo hizoambazo huimbwa mitaani au shuleni, zina maudhui mbali mbali. Aidha, kupitia tafiti hizo, tumebaini kwamba nyimbo za michezo ya watoto,

kama tanzu nyingine za fasihi simulizi, zinaenda sambamba na jamii zinavyoimbwa. Kwa hivyo hubadilika kulingana na mabadiliko yanayotokea katika jamii. Hii ina maana kwamba wakati wa ukoloni nyimbo za michezo ya watoto ziliakisi hali iliyokuwepo wakati huo. Kwa muktadha huo, bila shaka utendaji, fani na maudhui yake ulibadilika kwa kujielekeza na hali halisi ya mfumo wa ukoloni. Hata hivyo, kazi tangulizi hizo hazijachunguza jinsi dhamira za nyimbo katika michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema.

## 2.3 Nadharia za Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili, nazo ni: Nadharia ya Uchambuzi Matini, na Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Nadharia zimejadiliwa na kuchambuliwa kama ifuatavyo.

### 2.3.1 Nadharia ya Uchambuzi wa Matini

Uchambuzi Matini iliasisiwa na Lassweu (1948) ni mkabala wa kinadharia ambao unajikita katika kuchunguza ubunifu wa msanii katika vipengele vya fani na maudhui katika kazi za sanaa kwa ujumla. Lengo la kazi ya sanaa huangaliwa kwa kuzingatia uhusiano uliopo wa kazi za fasihi katika vipengele tofauti vya kifani. Uhakiki huu unazingatia upeo wa msomaji atakavyoifasiri matini kwa kurejelea muktadha na historia ya jamii iliyokusudiwa ilikupata athari za kazi hiyo kama vile mwamko, kuburudisha nakadhalika. Mkabalahuu ulikusudiwa kuchunguza falsafa, ubunifu wa mwandishi, historia na mambo ya kiutamaduni. Hii ilikuwa ni chanzo cha kuzaliwa kwa nadharia mbalimbali za fasihi.

Maendeleo ya kijamii na kiutamaduni katika karne ya 20 yameitanua nadharia hii katika nchi nyingi kama vile Ulaya, Amerika ya kati na Afrika ya Kusini. Kwa mujibu wa Jabish (2012) uchambuzi wa matini ni mbinu ya kisayansi ya jamii ambayo matini inahakikiwa kwa kuangaliwa maana, utunzi na uhalisi. Lassweu(1948) ametoa maswali ya kujiuliza wakati wa uchanganuzi wa matini nayo ni: Nani amesema nini, amelengwa nani, kwa nini, kwa kiwango gani kazi inaathiri hadhira iliojengwa?

Misingi mikuu ya nadharia hii imejengwa katika wazo kuwa fasihi hutumia lugha ambayo ndio nyezo yake kuu. Fasihi hutumia vionjo tofauti ambavyo huitofautisha kazi ya fasihi na kazi nyingine zisizo za kifasihi. Hivyo ni kazi ya mhakiki kuchambua vipengele hivyo. Maana ya kazi ya fasihi yaani maudhui, falsafa, ujumbe na mafunzo hupatikana baada ya mhakiki kuvichambua vipengele vyake na sio kuchukulia maana ya juu au ya kikamusi kama inavyojitokeza katika matini inayohakikiwa.Pia, katika nadharia hii, uchambuzi wa kazi ya fasihi huweza kutofautianakulingana na elimu, ujuzi na uwelewa wa mhakiki wa kazi hiyo. Kazi ya sanaa nilazima iathiriwe na mambo yaliomo katika jamii kama vile siasa. Hivyo, mtunzi huathiriwa na hali hiyo kwani ndimo anamoishi na hawezi kuepuka na ndio sababu hujitokeza katika kazi zake kwani muktadha hubeba maudhui ya kazi ilioandikwa. Fani ni lazima ioane na maudhui yanayosawiriwa katika kazi ya fasihi. Kazi yafasihi ikizidi kipengele kimoja na kingine huwa dhaifu na kazi hiyo huonesha udhaifu huo. Hii ina maana kwamba kazi ya fasihi inapoegemea kuwa na fani dhaifu au maudhui yakiwa dhaifu kazi hiyo yote huonesha udhaifu huo. Pia, fani inapokuwa nzuri na maudhui yakiwa dhaifu, udhaifu huo pia hujitokeza katika kazi na pia

kinyume chake. Kazi ya fasihi huwa na hadhira maalumu ambayo hulengwa kupata na kuathiriwa naujumbe wa msanii kupitia kazi ya fasihi, kinyume chake lengo la msanii hushindwa kufikiwa. Nadharia ya uchambuzi wa matini itatumika kuhakiki kipengele chafani na kuibua dhamira zinazopatikana katika nyimbo za michezo ya watoto kwakuangalia nani anaongea nini na athari yake kwa hadhira yake iliyokusudiwa. Udhaifu wa nadharia hii ni imejikita zaidi kulijibu lengo mahususi la kwanza na kutotosheleza kulijibu lengo mahususi la pili na la tatu.

### 2.3.2 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Hii ni nadharia ya kifasihi inayojikita katika kumuangalia msomaji (hadhira) na uzoefu wake wa kazi za kifasihi. Nadhariaya mwitiko wa msomaji, iliasisiwa na Stanley Fish (1980), Jane Tompkins (1980)na Wolf Gang Isser (1974), ambao ni Wajerumani. Wataalamu hao wanaeleza kuwa kazi ya fasihi inapaswa kutazamwa kulingana na mila nadesturi, au utamaduni wa msomaji. Hii ni kwa sababu msomaji ana uhuru wa kutafsiri kama aonavyo kutokana na uzoefu wake na si kutokana na uzoefu wa mwandishi.Wanaendelea kusema kuwa, kazi ya fasihi inajikita katika ishara na taswira mbalimbali. Kwa hivyo, kutokana na taswira na ishara hizo, matini za kifasihi huwa hazina maana moja bali zinakuwa na maana zaidi ya moja. Wananadharia hawa huona kazi ya fasihi kuwa ina mapengo mengi ambayo yanamlazimisha msomaji kuyaziba. Katika kuyaziba msomaji atajikuta ametunga matini nyengine mpya inayotokana na matini ile asilia, kwa hivyo kazi kubwa yamsomaji ni kusoma kazi kwa ufatiliaji wa hali ya juu kabisa, na hatimae kufasili kazi hiyo kutokana na uzoefu pamoja na uwezo wake. Hivyo nadharia hii hasa ndio

ilimvuta mtafiti katika kuchambua data kwa vile ilikuwa haina mipaka maalumu katika uchambuzi wake.

Misingiya nadharia hii ni kwamba kazi ya sanaa, hurejelea kazi inayosomwa kwa tafsiri ili ithibitishwe kwamba kazi hiyo inaafikiana na yale yanayo kumbukwa na msomaji wa kazi za fasihi. Vile vile, hubainisha jinsi miktadha ya matini isiohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji. Pia, hudhihirisha kuwamaoni ya msomaji yanafungamana na mada muhimu za hadithi Wamitila (2002).

## 2.4 Muhutasari wa Sura ya Pili

Katika sura hii mtafiti amebainisha na kujadili dhana muhimu zilizotumika katika utafiti huu, ambazo ni asili ya nyimbo, maana ya nyimbo na uanishaji wa nyimbo.Pia, nyimbo za michezo ya watoto na asili yake, dhana ya maadili na umuhimu wake vimefafanuliwa. Dhana ya fanina maudhui imejadiliwa kwa kujikita zaidi katika kipengele cha maadili ya jamii. Mwisho wa sura hii ni ufafanuzi wa nadharia zilizotumika kuongoza uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti huu. Sura inayofuata inahusiana na mbinu na zilizotumika katika utafiti huu.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mbinu za utafiti zilizotumika katika mchakato wautafiti huu, kuanzia mwanzo wa ukusanyaji wa data hadi mwisho wa uchambuzi na uwasilishaji wa data katika tasnifu hii. Katika sura hii, mambo yanayojadiliwa ni  mkabala wa utafiti, vyanzo vya data vilivyotumika katika utafiti huu, njia, mbinu, zana na vifaa vya kukusanyia data,sampuli iliyotumika na eneo la utafiti. Mwishoni mwa sura hii inaonesha uchambuzi wa data ulivyofanyika, ukubalifu wa data na itikeli ya utafiti.

## 3.2 Mkabala wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaelezo katika uchambuzi na uwasilishaji wa data kuhusu uchunguzi wa dhamira za nyimbo za watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema katika jamii ya Wazanzibari. Mbinu za ukusanyaji wa data kama vile, ushuhudiaji, usaili na mahojiano zilitumika katika ukusanyaji wa data za utafiti. Kwa hivyo, mtafiti aliorodhesha na kuhakiki nyimbo za michezo ya watoto ili kuchambua dhamira zilizomo katika nyimbo hizo. Aidha, mtafiti alionesha jinsi dhamira hizo zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema watoto.

## 3.3 Aina ya Utafiti

Utafiti huu ni wa uwandani ambapo data za msingi za utafiti zilikusanywa kutoka maeneo yaliyobainishwa katika utafiti huu. Kama mtafiti alivyobainisha katika kipendele 3.2 hapo juu, utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaelezo katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Mtafiti ameamua kutumia aina hii ya utafiti kwa mujibu wa

malengo na madhumuni ya utafiti, asili ya tatizo na asili ya data zilizokusanywa. Kwa mujibu wa Kothari (2009) tafiti za kimaelezo hazihitaji kiwango kikubwa cha uthabiti na upangiliwaji wake. Hivyo, mtafiti alitumia aina hii ya utafiti ili kufikia malengo mahsusi ya utafiti.

### 3.4 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika Wilaya ya Kaskazini B, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Tanzania. Wilaya ya Kaskazini B ina shehia ishirini na nne za kiutawala ambazo ni Donge Karange, Donge Kipange, Donge Mbiji, Donge Mchangani, Donge Mnyimbi, Donge Mtambile, Donge Vijibweni, Fujoni, Kilombero, Kinduni, Kiomba Mvua na Kitope. Pia kuna shehia za Kiwengwa, Mahonda, Makoba, Manga Pwani, Mgambo, Misufini, Mkadini, Muwanda, Pangeni, Upenja na Zingwe Zingwe.Shehia zilizoteuliwa katika utafiti huu pamoja na shule zake kwenye mabano ni Shehia ya Mahonda (Shule ya Msingi Mahonda), Shehia ya Kindundi (Shule ya Msingi Kinduni) na Shehia ya Donge Mtambile (Shule ya Msingi Mtambile). Mtafiti aliteua shehia hizi kwa madhumuni maalumu kwa sababu nyimbo za michezo ya watoto zimeshamiri sana katika maeneo haya. Aidha, maeneo hayo yamo pembezoni mwa mji na mtafiti aliweza kuyafikia kwa urahisi ambapo wakazi wa maeneo hayo walihusishwa kama wahojiwa wa utafiti huu.

### 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Sehemu hii inafafanua sampuli na jinsi uteuzi wa sampuli ulivyofanyika katika utafiti huu wakati wa ukusanyaji wa data.

### 3.5.1 Sampuli

Sampuli ni vitafitiwa au wahojiwa waliochaguliwa kwa ajili ya kuwakilisha utafiti au wahojiwa wengine wa aina hiyo kutoka katika kundi kubwa. Usampulishaji nimpango wakuchagua sampuli maalumu kutoka katika kundi kubwa (Kothari 2004:55-56). Amini (2005:236) anafafanua kuwa sampuli hupatikana kwa kuchagua sehemu tu kutoka katika kundi kubwa na matokeo yake yanaweza kujumuishwa kwa kundi lote la wahojiwa. Sampuli lazima iwakilishe wahojiwa kama itakavyowezekana ambapo sifa zote za kundi hilo zipatikane katika sampuli iliyochaguliwa kulingana na mada ya utafiti unaohusika, kwa mfano jinsi, kiwango cha elimu nakadhalika.

Sampuli ya utafiti huu ni

a) Nyimbo za michezo ya watoto wa Wilaya ya Kaskazini B, Mkoa wa Kaskazini Unguja;
b) Watoto wenye umri wa miaka 4-12 kutokaWilaya ya kaskazini B, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

### 3.5.2 Usampulishaji

Nussu (2012:41) anaeleza kwamba ni vigumu kwa mtafiti kushughulikia idadi kubwa ya wahojiwa wanaoshiriki katika utafiti hatakama anavutiwa na wanajamii hao. Mtafiti hutakiwa kuchagua idadi maalumu ya wanajamii wa kushughulikia katika utafiti wake. Idadi hiyo ya wanajamii lengwa,mtafiti alichagua wanafunzi (21) kwa kutumia usampulishaji nasibu 7 kutoka kilashule iliyoteuliwa kuwa sampuli ya utafiti, yaani Mahonda, Kinduni na Mtambile.

Wahojiwa hawa wameimba nyimbo mbalimbali za michezo ya watoto ambapo wazazi na walimu wao wamezitolea ufafanuzi. Hivyo basi,utafiti huu umetumia sampuli ya:

a) Nyimbo 20 za michezo ya watoto watoto wa Wilaya ya Kaskazini B, Mkoa wa Kaskazini Unguja. Nyimbo hizi ziliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa. Mtafiti aliteuwa nyimbo kwa kuamini kuwa zingempatia datana taarifa za kumsaidia kujibu maswali ya utafiti wake. Nyimbo hizi pia zimetumika kama vyanzo vya data na taarifa za msingi zilizowezesha mtafiti kujibu maswalikatika tasnifu hii.
b) Watoto 21 wenye umri wa miaka 4-12 kutokaWilaya ya kaskazini B Mkoa wa Kaskazini Unguja;

Jadweli lifuatalo linaonesha idadi ya watafitiwa

| Watafitiwa | Mahonda | | Kinduni | | Mtambile | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W’ke | W’ume | W’ke | W’ume | W’ke | W’ume | |
| Wanafunzi | 3 | 4 | 4 | 3 | 3 | 4 | 21 |
| Walimu | 1 | 1 | 2 | - | 1 | 1 | 6 |
| JUMLA KUU | 4 | 5 | 6 | 3 | 4 | 5 | 27 |

### 3.7 Ukusanyaji wa data

### 3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu za ukusanyaji wa data zilizotumika katika utafiti huu ni ushuhudiaji, usaili na majadiliano ya vikundi. Mtafiti ameona ni vizuri kutumia mbinu hizi kwa sababu utanzu huu ni wakifasihi na hupatikana kwa kuchezwa, kughaniwa na kuimbwa. Pia, watu wanaozitumia nyimbo hizi ni watoto waliopo majumbani na mashuleni ambao baadhi yao hawajui kusoma na kuandika.

#### 3.6.1 Mbinu ya Ushuhudiaji

Katika utafiti, ushuhudiaji ni mbinu moja wapo ya ukusanyaji wa data ambayo mtafiti hufika mahali ambapo taarifa za utafiti zinapatikana ili kupata taarifa hizo kwa kushuhudia mwenyewe (Kothari, 2009: 96). Katika utafiti huu, mtafiti alitembelea maeneo mbali mbali ambamo nyimbo za michezo ya watoto huimbwa kwa madhumuni ya kukusanya data.

Mbinu ya ushuhudiaji ilitumika kwa mtafiti kutembelea mahali penye mikusanyiko ya watoto kama vile mitaani na mashuleni. Mbinu hii ilitumika kukusanya data kuhusu lengo la kwanza la utafiti ambalo lililenga kubainisha nyimbo za michezo ya watoto. Kwa hiyo, data zilizokusanywa kwa mbinu hii zilifanikisha kufikia lengo mahususi la kwanza la utafiti huu.

#### 3.6.2 Mbinu ya Usaili

Mbinu hii huhusisha maswali ya ana kwa ana ambayo mtafiti anapata taarifa kwa kukutana na wahojiwa kama walimu, wanafunzi, nakadhalika. Mtafiti alibadilishana mawazo na wahojiwa na kuwauliza maswali ya ana kwa ana baina yao. Katika usaili, mtafiti hueleza lengo la utafiti wake na kitu anachohitaji kutoka kwa wahojiwa (Amin 2005:178). Mtafiti alikwenda kuonana na wahojiwa ambao wanazijua baadhi

ya nyimbo za michezo mbalimbali ambao walitoamaelezo yaliyohitajika. Mtafiti alitumia mbinu hii kwa kuwauliza wahojiwa kuhusu matumizi ya nyimbo za michezo ya watoto na maudhui ya nyimbo hizo. Mbinu hii ilimuwezesha mtafiti kupata taarifa za kina juu ya mada yake. Data zilizopatikana zilisaidia kufikia lengo mahususi la pili la utafiti huu. Sababu za kutumia mbinu tatu tofauti ni kupata uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti.

### 3.6.2 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi

Kothari (2009) anaeleza kuwa majadiliano ya vikundi ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo inahusisha maswali na majibu yanayoendesha mazungumzo ya ana kwa ana baina ya mtafiti na wahojiwa. Faida za kutumia mbinu ya majadiliano ni kwamba inarahisisha kupata maelezo ya kina au data za moja kwa moja kutoka kwa wahojiwa. Mbinu hii pia ni nzuri kwa wahojiwa ambao hawajui kusoma wala kuandika, ilitumika kuwahoji wahojiwa ambao ni mchanganyiko; waliosoma na wasiosoma. Mbinu hii ilitumika kupata data kuhusu dhamira za nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga watoto ujasiri na tabia njema. Data zilizokusanywa kupitia mbinu hii zilifanikisha kufikia lengo mahususi la tatu la utafiti huu.

## 3.7 Uchanganuzi wa data

Kothari (2004:18 - 122) anasema kuwa baada ya kukusanya data mtafiti anapaswa kuzichakata na kuzichambua data kwa kurejelea malengo ya utafiti. Uchambuzi waData hufanyika kwa kupitia hatua kadhaa kama vile uwekaji wa misimbo,majadweli, uhariri na inapolazimu kunakuwa na uchoraji wa michoro ya kitakwimu kwa lengo la kuyafupisha maelezo. Utafiti huu ulitumia mkabala wa

kimaelezo katika kuchambua na kuzichakata data zilizokusanywa. Mkabala huu ulitumika kwasababu data ni matini za fasihi na uchambuzi wake ni wa maelezo.

## 3.8 Uthabiti na ukubalifu wa data

Katika sehemu hii, mtafiti anabainisha na kujadili uthabiti na ukubalifu wa data iliyotumika katika utafiti huu.

### 3.8.1 Uthabiti na Ukubalifu wa Data

Moja ya sifa kuu ya data ni uthabiti wa data zilizopatikana. Sigh (2007) anaeleza kuwa mbinu zote zilizotayarishwa kwa ajili ya kufanyia utafiti lazima zipimwe kuona kama zinafaa kutumika katika mazingira halisi yaliyokusudiwa. Mtafiti atayapima maswali kwa watu wasio walengwa lakini ambao wanafanana na walengwa wa utafiti kabla ya data za utafiti kukusanywa. Lengo kuu lilikuwa ni kuyapima maswali ili kuona kwamba yanajibika. Pia, kuona iwapo mtafiti anaweza kupata taarifa au data anazozitarajia kwa mujibu wa utafiti wake.

### 3.8.2 Kukubalika kwa Data za Utafiti

Mligo **(**2012**)** anaeleza kuwa kuaminika kwa data za utafiti hutokana na uwezo wa mbinu za utafiti wa kutoa matokeo yale yale yaliyokusudiwa kwa kutumia mbinu hizo. Kukubalika kwa data ni pale panapokuwa na uhusiano kati ya taarifa zilizotolewa na watu wale wale kwa muda tofauti. Katika utafiti huu, kukubalika kwa data za utafiti kulikuwa ni kuhakikiwa kwa mbinu ambazo mtafiti alizitumia katika ukusanyaji wa data na kuona kwamba data zimetoa matokeo yaliyotarajiwa.

## 3.9 Vifaa vya Utafiti

Kwa kuzingatia mbinu zilizotajwa hapo juu, utafiti ulitumia vifaa vilivyoendana na mahitaji ya ukusanyaji wa data. Vifaa hivyo vilikuwa kalamu, penseli na karatasi, ambavyo vilitumika kuandikia data zilizokusanywa kutoka maktabani na uwandani kwa lengo la kuweka kumbukumbu zilizosaidia katika uandishi wa utafiti wenyewe. Pia kompyuta na kinyonyi vilitumika kuwekea kumbukumbu na kucharazia kazi kutoka mwanzo hadi mwisho wa utafiti.

## 3.10 Itikeli ya Utafiti

Mligo (2012) anaeleza kuwa itikeli au maadili ni kanuni zilizowekwa na kukubaliwa na jamii ili kuongoza mwenendo wa maisha na tabia halisi ya maisha ya wanajamii inayohusika. Katika utafiti, itikeli inahusu haki ya mhojiwa kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni ya utafiti na haki ya kupata matokeo ya utafiti. Pia, mhojiwa ana haki ya kujibu maswali aliyopewa kujibu na haki ya kuridhia au kukataa kushiriki katika utafiti. Aidha, katika utafiti huu, mtafiti alifuatilia kibali cha utafiti kutoka mamlaka inayohusika ili kuhakikisha kwamba utafiti unafanyika kwa kufuata kanuni na taratibu za nchi. Vilevile, mtafiti alitunza siri za wahojiwa wake ikiwa ni pamoja na maelezo na mahojiano yaliyofanyika wakati wa utafiti.

## 3.11 Muhutasari wa Sura ya Tatu

Katika sura hii mtafiti amebainisha mbinu za utafiti zilizotumika katika mchakato wa utafiti huu, kuanzia mwanzo katika ukusanyaji wa data hadi mwisho wakati wa kuandika tasnifu hii. Katika sura hii, mambo yanayojadiliwa ni vyanzo vya data vilivyotumika katika utafiti huu, njia, mbinu, zana na vifaa vya kukusanyia data, sampuli iliyotumika na eneo la utafiti. Mwishoni mwa sura hii inaonesha namna

uchambuzi wa data ulivyofanyika, ukubalifu wa data na itikeli ya utafiti. Sura inayofuata inahusu uchambuzi na uwasilishaji wa data.

# SURA YA NNE

# 4.0 UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uchambuzi na uwasilishaji wa data na kujadili matokeo ya utafiti kuhusu dhamira za nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema katika jamii ya Wazanzibari. Uchambuzi na uwasilishaji wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti huu. Aidha, inaonesha namna utafiti unavyohusiana na nadharia iliyotumika kuongoza uchambuzi wa data na mwisho, sura hii inaishia na hitimisho la mjadala wa matokeo ya utafiti. Kabla ya uchambuzi wa data yafuatayo ni maelezo mafupi ya taarifa za wahojiwa wa utafiti.

## 4.2 Taarifa za Wahojiwa

Taarifa za awali za wahojiwa zilizojadiliwa katika utafiti huu ni jinsia, umri na kiwango cha elimu cha wahojiwa kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Jinsia ya Wahojiwa

Mtafiti alizingatia uwiano na usawa wa kijinsia wakati wa ukusanyaji data kutoka kwa wahojiwa aliowalenga. Hii imefanyika ili kubeba mawazo ya jinsia zote mbili kwa maana ya wanawake na wanaume ili kuondoa dhana ya mfumo dume wa kuhoji aina moja tu ya jinsia na kuisemea jinsia nyingine.

### 4.2.2 Umri wa Wahojiwa

Data kutoka eneo la utafiti zinaonyesha kuwa watafitiwa walikuwa wa kuanzia miaka 4 hadi 50. Kundi ambalo limechukua idadi kubwa katika utafiti huu ni umri kuanzia miaka 4 – 9. Kundi hili limekuwa na wahojiwa wengi kwa sababu utafiti

ulikusudia watoto wadogo ambapo wengi ni wanafunzi wa shule za msingi na maandalizi. Katika umri wa miaka 4 – 9 huu ndio umri ambao watoto wengi walau wanakuwa na uwezo wa kuimba na kucheza michezo mbalimbali wao wenyewe. Hili lilikuwa kundi muhimu sana kwa mtafiti kwa kuwa ni rahisi kuimba nyimbo mbalimbali. Kundi jingine lilikuwa ni la walimu ambao walikuwa na umri kuanzia miaka 25 hadi 50. Walimu walitumika katika vikundi vya majadiliano kuhusu jinsi dhamira za nyimbo katika michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema.

### 4.2.3 Elimu ya Wahojiwa

Elimu inamsaidia mtu kuwa na uelewa wa kuelezea jambo au mambo kwa upana na usahihi zaidi. Katika kuzingatia hilo, mtafiti alitaka kupata watu wenye viwango mbalimbali vya elimu kuanzia wale ambao wana elimu ya ngazi ya chini yaani stashahada mpaka ngazi ya juu. Kiwango cha elimu kilizingatiwa katika wapata wahojiwa walimu pekee kwa sababu mchanganyiko wa ngazi za elimu huleta uwiano sawa wa taarifa na maarifa ya kiutafiti.

## 4.3 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Katika sehemu hii mtafiti amewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa juu ya dhamira za nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema katika jamii ya Wazanzibari. Ili kufikia lengo kuu, utafiti huu umeongozwa na malengo mahususi matatu ambapo lengo la kwanza lililenga kubainisha nyimbo za michezo ya watoto, mantiki na miktadha ya uimbaji katika jamii ya Wazanzibari. Lengo la pili lilikuwa kuchambua dhamira za nyimbo za michezo ya watoto katika

jamii ya Wazanzibari. Lengo la tatu, lilikusudia kuonesha jinsi dhamira hizo zinavyosaidia kujenga ujasiri na tabia njema katika jamii ya Wazanzibari.

### 4.3.1 Nyimbo za Michezo ya Watoto, Mantiki na Miktadha ya Uimbaji

Katika sehemu hii mtafiti anakusudia kujadili lengo mahususi la kwanza la utafiti huu ambalo lililenga kubainisha nyimbo za michezo ya watoto, mantiki na miktadha ya uimbaji katika jamii ya Wazanzibari. Data za utafiti kuhusu lengo hili zilikusanywa kwa kutumia mbinu za ushuhudiaji. Mtafiti alikusanya data za uwandani kutoka kwa wahojiwa ili kupata majibu ya maswali yaliyolenga kufikia lengo la kwanza. Baada ya kufanya ushuhudiaji, mtafiti aliweza kubainisha nyimbo zifuatazo:

#### 4.3.1.1 Duara

Huu ni wimbo unaoimbwa katika mchezo ambao washiriki wake huwa ni zaidi ya watano. Mchezo huu huchezwa kwa kujipanga duara huku washiriki wakiwa wamekamatana mikono.Katika kufanya hivyo, watoto huzunguka kwa mwendo wa haraka na wakiwa wanaimba wimbo ufuatao:

1. *Duara duara hili ni duara*
   *Mwenzetu hayupo katika duara*
   *Tukamtafute tukamkamate*
   *Kisha tumlete katika duara*
   *Na dada Aisha aingie kati*
   *Aoneshe mbwembwe*
   *Katika duara.*

Mantiki ya wimbo huo ni kwamba watoto katika jamii wanatakiwa wawe na tabia ya kujaliana na kuthaminiana ikitokezea mmoja wao hayupo waweze kumtafuta.

Wimbo huu unalenga kukuza umoja na ushirikiano katika jamii husika. Hivyo jamii inaadilishwa iachane na tabia ya kuishi kwa utengano badala yake iishi katika hali ya umoja na ushirikiano.

#### 4.3.1.2 Moja Mbili Tatu

*Moja mbili tatu* ni wimbo unaoimbwa katika mchezo wa watoto ambapo washiriki wanaoimba wimbo huu ni wanafunzi darasani. Mwalimu au mwanafunzi mmoja huanza kuimba wimbo na wengine wakaitikia.Wimbo wa *Moja mbili tatu* huimbwa kama ifuatavyo:

*2. Moja mbili tatu nne tano*
*Nilipata samaki mkubwa mno*
*Na yule mwenye nguvu*
*Kwanini akamuachia*
*Kanikata kidole*
*Nalia iiii mama nalia iiii*

Mantiki ya wimbo huo kwanza ni kuwajenga watoto ujasiri wa kuwa na uwezo wa kuhesabu vitu mbali mbali. Pia, watoto wanatakiwa wawe makini wanapovua samaki wakubwa bahari. Wimbo huu unalenga kukuza hali ya tahadhari kwa watoto na kuwataka wawe makini katika harakati zao za maisha kila siku ili waweze kuepukana na mabalaa ya aina mbalimbali.

#### 4.3.1.3 Mpilipili

*Mpilipili* ni wimbo ambao huimbwa katika michezo ya watoto ambapo waimbaji ni watoto wenye umri tofauti hususani umri wa kuanzia miaka 7 hadi 12. Kwa kawaida,

wimbo huu huimbwa na watoto wanapocheza wakiwa nyumbani au shuleni. Wimbo wa *Mpilipili* huimbwa kama ifuatavyo:

3. *Mpilipili mti gani wa kuinama inama aaaa*
   *Inama mimi nasema na wewe wanishikia matama aaaaa*
   *Inama mgeni akija eee*
   *Tumpokee Inama mgeni akija ee Tumpokee Inama*

Mantiki ya wimbo huu ni kuwajenga watoto kuwa na heshima kwa wakubwa zao katika maisha yao ya kila siku. Hivyo basi, watoto wanapaswa kuwa na heshima kwa wageni waliofika nyumbani kwao. Kupitia wimbo huu, watoto hujengwa wawe na tabia ya kuwasalimia wageni kwa heshima ikiwa ni pamoja na kuwalaki wageni waliotembelea nyumbani kwao. Kwa ujumla, tabia hii huwasaidia watoto kukua katika malezi na maadili mema ambayo hudumu nayo hadi katika maisha ya utu uzimani.

#### 4.3.1.4 Panya

*Panya* ni wimbo unaoimbwa katika michezo ya watoto wakati wa jioni wakiwa wanacheza mtaani au nyumbani. Watoto wenye umri kati ya miaka 7 hadi 14 hujipanga duara ambapo mmoja huanza kuimba wimbo na wengine wakaitikia huku wakiwa wanachezesha miguu kwa kupigapiga chini. Wimbo wa *Panya* huimbwa kama ifuatavyo:

4. *Panya watatu vipofu*
   *Walikwenda kwa mke wa mkulima*
   *Wakamkata mkia kwa kisu kikali parampara*
   *Parara parara mpara parara*

Mantiki ya wimbo huo ni kuwajenga watoto ujasiri katika harakati za maisha yao ya kila siku bila kujali hali zao za kimaumbile. Hii ni kwa sababu katika jamii wamo watu ambao wanabweteka kuwa ombaomba kutokana na hali zao za kimaumbile. Hivyo basi, panya watatu vipofu wanaashiria watoto wenye ulemavu wa macho ambao wanapambana katika harakati za maisha yao ya kila siku bila kujali hali ya ulemavu walio nao.

#### 4.3.1.5 Maji ya Mto

*Maji ya mto* ni wimbo unaoimbwa katika michezo ya watoto nyakati za jioni wakiwa wanacheza mtaani au nyumbani. Watoto hujipanga mstari ambapo mmoja huanza kuimba na wengine wakaitikia huku wakiwa wanatembea kwa kwenda mbele na kurudi nyuma. Wimbo wa *Maji ya mto* huimbwa kama ifuatavyo:

5. *Maji ya mto yanakwenda*
   *Yanakwenda mbele kwa mbele*
   *Yanarudi nyuma kwa nyuma*

Mantiki ya wimbowa Maji ya mto ni kuwajenga watoto ujasiri wa kuvuka mito kutoka ng’ambo moja kwenda nyingine. Pia, watoto wanatakiwa wachukue hadhari wakati wanapoogelea au kuvuka mito kwa sababu maji yamto ya mkondo ambao wakati mwingine humsukuma mtu mbele na wakati mwingine humrudisha nyuma. Wimbo huu unakusudia kukuza hali ya tahadhari kwa watoto wanapokuwa katika harakati zao za maisha ya kila siku.

#### 4.3.1.6 Nalia

*Nalia* ni wimbo unaoimbwa katika michezo ya watoto wakati wa jioni wakiwa wanacheza mitaani. Wimbo huu huimbwa na wasichana wanapokuwa wanacheza

peke yao ambapo wasichana kati ya 6 hadi 9 hujipanga mstari ambapo mmoja huanza kuimba na wengine wakaitikia huku muimbaji akiwa anatembea kwa katika kikundi. Wimbo wa *Nalia* huimbwa kama ifuatavyo:

6. *Mwenzenu minalia minalia minalia*
   *Walilia kitu gani kitu gani kitu gani*
   *Nalilia sina shoga sina shoga sina shoga*
   *Tafuta shoga ako shoga ako shoga ako*
   *Anacheza na shoga akee kwa raha zake x2*

Wimbo wa *Nalia* unakusudiwa kuwajenga watoto tabia njema ya kujua umuhimu wa marafiki katika maisha ya kila siku. Aidha, wimbo huu huwajenga watoto kuwa na tabia ya kutafuta marafiki ambao atashirikiana nao katika shughuli mbalimbali. Hii ni kwa sababu mtu anapokosa marafiki katika jamii huwa kama vile ametengwa na jamii yake. Hivyo basi, kutokana na umuhimu wa rafiki, mtoto anapaswa kulia iwapo atakosa rafiki na anapaswa kufanya biidi kuhakikisha kwamba amepata rafiki.

#### 4.3.1.7 A,e,i,o,u

*A, e, i, o, u* ni wimbo mmojawapo unaoimbwa katika michezo ya watoto ambapo washiriki wanaoimba wimbo huu ni wanafunzi darasani. Wanafunzi wa madarasa ya awali na msingi chini wenye umri baina ya miaka 4 hadi 8 ndio aghalabu huimba. Mwalimu huanza kuimba wimbo na wanafunzi wakaitikia. Wimbo wa *a, e, i, o, u* huimbwa kama ifuatavyo:

7. *A – Allahuwa Allah*
   *E – Ewe mola wetu*
   *I – Ibariki dua yetu*
   *O – Ombi letu sisi*

*U – Utujaalie*
*Tuwe na afya tuweze kucheza*

Mantiki ya wimbo huo ni kuwajenga watoto ujasiri wa kuwa na uwezo wa kuzitamka na kuzielewa irabu za lugha ya Kiswahili. Aidha, kupitia wimbo huo watoto wanajengwa imani ya kuwa maombi yao yote waombe kwa Mwenyezi Mungu mtukufu. Pia, wimbo huo unaonesha umuhimu wa kuwa na afya njema kwa watoto kwa sababu watoto wanajengwa Imani kuwa ili waweze kucheza ni lazima wawe na afya njema. Hivyo, unalenga kuwakuza watoto katika hali ya tahadhari kwa kuwataka wawe makini katika harakati zao za maisha kila siku ili waweze kuepukana na maradhi ya aina mbalimbali.

#### 4.3.1.8 Tuamkapo asubuhi

*Tuamkapo asubuhi* ni wimbo ambao huimbwa katika michezo ya watoto katika muktadha wa nyumbani au darasani. Wimbo huu huimbwa na watoto wa kike na kiume wenye umri kati ya miaka 6 hadi 12. Mtoto mmoja ambaye aghalabu huwa ndiye kiongozi wa kikundi huanza kuimba wimbo na wengine wakafuatia. Wimbo wa huu huimbwa kama ifuatavyo:

8. *Tuamkapo asubuhi*
   *Tuwasalimie wazazi*
   *Shikamoo baba shikamoo mama*
   *Hiyo ndio tabia njema*

Mantiki ya wimbo huo ni kuwajenga watoto kuwa na tabia njema ya kuwasalimia wazazi wao kila waamkapo asubuhi. Pia, wimbo huo unawaonesha watoto umuhimu

wa tabia ya kuwasalimia wazazi pamoja na wakubwa wao kila wanapoamka au wanapokutana nao kwa siku.

#### 4.3.1.9 Kidabwada

*Kidabwada* ni jina la wimbo ambao huimbwa katika michezo ya watoto, wakati wa jioni wakiwa wanacheza mtaani au nyumbani. Watoto wa kike na kiume wenye umri kati ya miaka 7 hadi 14 hujipanga duara ambapo mmoja huimba wimbo na wengine wakaitikia huku wakiwa wanafuatisha vitendo vinavyoelezwa na kiongozi wao kupitia wimbo huu kama vile kukamata kichwa, mabega, tumbo pamoja na kucheza. Wimbo wa *Kidabwada* huimbwa kama ifuatavyo:

9. *Kidabwada mkia kamata*
   *Kamata kichwa kamata*
   *Kamata mabega kamata*
   *Kamata tumbo kamata*
   *Cheza chakacha chakacha chakacha*

Mantiki ya wimbowa huo ni kuwajenga watoto ujasiri wa kufanya mazoezi ya viungo ili wawe imara katika miili yao. Hii ni kwa sababu wimbo huo huambatana na vitendo ambavyo humfanya mtoto achangamke mwili kwani hucheza mpaka wakawa wanaloa jasho. Wimbo huu unakusudia kuwakuza watoto katika hali ya kuwachangamsha kimwili na kiakili. Hali ambayo huwajenga kuwa imara katika shughuli zao za kila siku za maisha.

#### 4.3.1.10 Turuke ruke

*Turuke ruke* ni jina la wimbo ambao unaimbwa katika michezo ya watoto ambapo aghalabu washiriki huwa ni wanafunzi darasani. Wanafunzi wa jinsia zote mbili

katika madarasa ya awali wenye umri kati ya miaka 4 hadi 6 ndio wanaoimba wimbo huu. Mwalimu huanza kuimba wimbo na wanafunzi wakaitikia huku wakiwa wanarukaruka kama wimbo unavyowaelekeza. Wimbo wa *Turuke ruke* huimbwa kama ifuatavyo:

*10. Turuke turuke turuke ruke*
*Turuke kama ndege wanavyoruka, turuke ruke*
*Turuke kama njiwa wanavyoruka turuke*
*Turuke kama chura wanavyoruka, turuke ruke*

Mantiki ya wimbo wa huo ni kuwajenga watoto ujasiri wa kufanya mazoezi ya kuchangamsha mwili ili wawe wachangamfu kimwili na kiakili. Hii ni kwa sababu wimbo huo huambatana na vitendo vya kurukaruka ambavyo humfanya mtoto achangamke. Wimbo huu unalenga kuwakuza watoto katika hali ya uchangamfu na kuepukana na ugoigoi wanapokuwa darasani. Hali hiyo huwajenga na kuwakuza katika hali ya uimara na uchangamfu katika shughuli za maisha yao ya ujana na utu uzima hapo baadaye.

#### 4.3.1.11 Unakwenda wapi

*Unakwenda wapi* ni wimbo wa michezo ya watoto ambao mara nyingi huimbwa wakati wa jioni watoto wakiwa wanacheza mtaani au nyumbani. Watoto wa kike na kiume wenye umri kati ya miaka 7 hadi 12 hujipanga duara ambapo mmoja huanza kuimba wimbo na wengine wakawa wanaitikia huku wakiwa wanapiga makofi. Wimbo wa *Unakwenda wapi* huimbwa kama ifuatavyo:

*11. Unakwenda wapi Darisalama*
*Kumsalimu nani baba na mama*

*Ukikutana nae umpe mkono*
*Acheche chechei aaa kidaa*

Kwa mujibu wa wahojiwa wetu, mantiki ya wimbo huu ni kuwajenga watoto tabia njema ya kujua umuhimu wa kuwasalimia wazazi, ndugu na jamaa katika maisha ya kila siku. Pia, wimbo huu huwajenga watoto kuwa na tabia ya kusafiri kwenda kuwaona na kuwasalimia wazazi kila baada ya muda pale ambapo wanaishi mbali na wazazi wao. Hii ni kwa sababu mtu anapoacha kwenda kuwaona na kuwasalimia wazazi huwa amejitenga na wazazi pamoja na ndugu zake katika jamii. Hivyo basi, kutokana na umuhimu wa wazazi, mtoto anapaswa kufanya biidi kuhakikisha kwamba anapata nafasi ya kwenda kuwaona na kuwasalimia wazazi kila baada ya muda fulani.

#### 4.3.1.12 Ndege kumi porini

*Ndege kumi porini* ni jina la wimbo unaoimbwa katika michezo ya watoto ambapo aghalabu washiriki huwa ni wanafunzi darasani. Wanafunzi wa jinsia zote mbili katika madarasa ya shule za awali na msingi wenye umri kati ya miaka 4 hadi 6 ndio huimba wimbo huu. Mwalimu au mwanafunzi aliyeteuliwa huanza kuimba wimbo na watoto wengine huitikia huku wakiwa wanarukaruka kama wimbo unavyowaelekeza. Wimbo wa *Ndege kumi porini* huimbwa kama ifuatavyo:

12. *Ndege kumi porini juu ya mti wamelala*
*Wamelalia furaha, furaha ya maisha*
*Wakwanza ameruka*
*Wapili akaruka*
*Watatu akaruka*
*Wanne akaruka*

*Watano akaruka*
*Wote wameruka wote wameruka*
*Wameruka juu kabisa*

Mantiki ya wimbohuo ni kuwajenga watoto ujasiri wa kufanya mazoezi ya kuchangamsha mwili ili wawe wachangamfu kimwili na kiakili wanapokuwa darasani. Hii ni kwa sababu wimbo huo huambatana na vitendo vya kurukaruka ambavyo humfanya mtoto achangamke. Wimbo huu unalenga kuwakuza watoto katika hali ya uchangamfu na kuepukana na ugoigoi wanapokuwa darasani pamoja na kuwajenga watoto hao katika stadi za kuzungumza, kusikiliza na kuhesabu. Aidha, wimbo huu huwajenga na kuwakuza katika hali ya uimara na uchangamfu katika shughuli za maisha yao ya ujana na utu uzima hapo baadaye.

#### 4.3.1.13 Watoto wazuri

*Watoto wazuri* ni wimbo ambao unaoimbwa katika michezo ya watoto, washiriki wanaoimba wimbo huu ni wanafunzi darasani. Wanafunzi wa madarasa ya awali na msingi chini wenye umri baina ya miaka 4 hadi 12 ndio aghalabu huimba. Mwalimu au mwanafunzi aliyemteua huanza kuimba wimbo na wanafunzi wakaitikia. Wimbo wa *watoto wazuri* huimbwa kama ifuatavyo:

*13. Sisi watoto wazuri, tucheze uwanjani*
*Tukiondoka uwanjani,tukimbilie nyumbani*
*Tusicheze barabarani,pamoja na misingini*
*Tusikubali kuitwa,kupewa pipi na pesa*
*Njiani kuna vibaka,hatari watatubaka*
*Hatudanganyiki.*

Mantiki ya wimbo huu ni kuwajenga watoto ujasiri wa kucheza ili wawe wachangamfu kimwili na kiakili wanapokuwa darasani. Aidha, wimbo huu unalenga kuwafunza watoto katika sehemu salama kama vile uwanjani na kuwataka wajiepushe kucheza katika maeneo ya hatari kama vile barabarani na misingini. Pia, wimbo huo unalenga kuwajenga tabia njema watoto hao ya kutokubali kuitwa wala kupokea zawadi kutoka kwa watu wasio wajua wanapokuwa wanacheza au wakiwa njia.

#### 4.3.1.14 Baba Kasafiri

*Baba kasafiri* ni wimbo wa michezo ya watoto ambao mara nyingi huimbwa wakati wa jioni, watoto wakiwa wanacheza mtaani au nyumbani. Watoto wa kike na kiume wenye umri kati ya miaka 7 hadi 12 hujipanga mstari mmoja ambapo huimba wimbo kwa pamoja huku wakiwa wanapiga makofi na kujirusha. Wimbo wa *Baba kasafiri* huimbwa kama ifuatavyo:

*14. Baba kasafiri baba kasafiri*
*Kasafiri kenda mrima*
*Kila hakumbuka x2*
*Hutaka nijirushe mzima mzima x2*

Kwa mujibu wa wahojiwa wetu, mantiki ya wimbo huu ni kuwajenga watoto tabia njema ya kujua umuhimu wa mzazi kuishi pamoja na familia yake katika maisha ya kila siku. Pia, wimbo huu huwatanabahisha watoto kuwa na tabia ya kurudi nyumbani wanaposafiri katika harakati za kutafuta maisha ili wasitelekeze familia zao. Hii ni kwa sababu mtu anaposafiri kwenda na mbali na familia yake na anapofika huko akasahau kurudi familia yake akiwemo mke na watoto hupata shida

sana. Hivyo basi, kutokana na umuhimu wa baba kuwa karibu na familia, mtu anapoishi mbali na familia yake anapaswa kwenda kuiona kila anapopata nafasi ili familia iweze kuishi kwa amani.

#### 4.3.1.15 Kificho

*Kijificho* ni wimbo katika michezo ya watoto ambao mara nyingi wakati wa jioni, watoto wakiwa mtaani au nyumbani hucheza mchezo wa kujificha. Mchezo huu huchezwa na watoto wa jinsia zote mbili wenye umri kati ya miaka 5 hadi 12 ambapo huimba wimbo baadaye wakakimbilia sehemu za kujificha kama vile nyumbani au majani makubwa karibu na nyumbani. Wimbo wa *Kijificho* huimbwa kama ifuatavyo:

*15. Kificho ficho*
*Banda jicho*
*Nawe unalo*
*Ilo jicho*
*Kajificheni*
*Fumba macho*
*Ukifumbua shauri yako.*

Mantiki ya wimbo huo ni kuwajenga watoto ujasiri wa kufanya mazoezi ya kuchangamsha mwili ili wawe wachangamfu kimwili na kiakili wanapokuwa. Hii ni kwa sababu wimbo huo huambatana na vitendo vya kurukaruka ambavyo humfanya mtoto achangamke. Wimbo huu unalenga kuwakuza watoto katika hali ya uchangamfu na kuepukana na ugoigoi wanapokuwa darasani pamoja na kuwajenga watoto hao katika stadi za kuzungumza, kusikiliza na kuhesabu. Aidha, wimbo huu

huwajenga na kuwakuza katika hali ya uimara na uchangamfu katika shughuli za maisha yao ya ujana na utu uzima hapo baadaye.

#### 4.3.1.16 Mnara wa baba

*Mnara wa baba* ni jina la wimbo wa michezo ya watoto ambao mara nyingi huimbwa wakati wa jioni ambapo watoto huwa wanacheza mtaani. Watoto wa kike na kiume wenye umri kati ya miaka 6 hadi 14 hujipanga duara ambapo huimba wimbo kwa pamoja huku wakiwa wanapiga makofi na kurukaruka. Wimbo wa *Mnara wa baba* huimbwa kama ifuatavyo:

*16. Mnara wa baba na mama njoo pwani njoo*
*Mnara wa baba na mama njoo pwani njoo*

Mantiki ya wimbohuo ni kuwajenga watoto ujasiri katika kufanya mazoezi ya kuchangamsha mwili ili wapate uchangamfu wa mwili na akili. Kwa sababu wimbo huo hufungamana na vitendo vya kupiga makofi na kurukaruka ambavyo humchangamsha mtoto. Wimbo huu pia, unalenga kuwakuza watoto katika hali ya uimara ili wasiwe legelege katika maisha yao ya kila siku. Hali hiyo huwakuza watoto katika hali ya umadhubuti katika shughuli za maisha yao ya hapo baadaye katika kipindi cha ujana hadi wanapokuwa watu uzima.

#### 4.3.1.17 Kasikazi

*Kasikazi* ni wimbo wa michezo ya watoto ambao aghalabu unaimbwa wakati wa jioni na usiku wa mapemba ambapo watoto wanakuwa wanacheza mtaani. Wimbo huu huimbwa na watoto wa jinsia zote mbili wenye umri kati ya miaka 6 hadi 12

hujipanga mstari mmoja na kuimba wimbo kwa pamoja. Wimbo wa *Kasikazi* huimbwa kama ifuatavyo:

17. *Kasikazi ndio kwetu mie*
    *Kizimkazi sikujui mie*
    *Akitoka baba namuona mie*
    *Mtu wa kazi nyumbani kwetu mie*
    *Hunipa zawadi ninyamaze mie*
    *Mmmmmh nanyamaza mie*

Mantiki ya wimbo huo ni kuwajenga watoto uzalendo wa kupenda makwao badala ya kupenda mahali kwa wati. Aidha, wimbo huu unawajenga watoto moyo wa kupenda kufanya kazi, hususani kazi za ndani za kuwasaidia wazazi wao kufanya kazi hizo.Wimbo huu pia, unalenga kuwakuza watoto katika hali ya kutunza siri katika maisha yao ya kila siku. Hali hiyo huwakuza watoto katika hali ya kutunza siri katika shughuli za maisha yao ya kila.

#### 4.3.1.18 Sukari ya Mahonda

*Sukari ya Mahonda* ni wimbo unaoimbwa katika michezo ya watoto shule na hata wakati wa jioni wakiwa wanacheza mtaani. Watoto wenye umri kati ya miaka 7 hadi 14 hujipanga duara ambapo mmoja huanza kuimba wimbo na wengine wakiitikia huku wakiwa wanacheza. Wimbo wa *Sukari ya Mahonda* huimbwa kama ifuatavyo:

18. *Sukari ya Mahonda inashira nyingi*
    *Anaeionja huanza vitimbi*
    *Ukijisahau tumbo litakuwa tumbwi*
    *Huwezi kucheza cheza huwezi kucheza cheza*

Mantiki ya wimbohuo ni kuwajenga watoto tabia njema ya kujali afya zao kutokana na matumizi ya sukari katika vyakula mbalimbali.  Aidha, wimbo huu unabainisha athari za sukari kama vile kuvimba mwili, kunenepa kulikopitiliza na kufanya kitambi.Pia wimbo huu, unalenga kuwakuza watoto katika hali ya kulinda na kutunza afya zao katika maisha yao ya kila siku. Hali ya kulinda afya dhidi ya magonjwa huwakuza watoto katika hali ya kuwa imara na kuwa wenye nguvu za kufanya kazi katika shughuli za maisha yao ya kila siku.

#### 4.3.1.19 Ndugu yetu

*Ndugu yetu* ni wimbo ambao huimbwa katika michezo ya watoto wakati wa jioni wakiwa wanacheza mtaani. Watoto wenye umri kati ya miaka 6 hadi 12 hujipanga mistari na kuanza kuimba wimbo huku wakiwa wanacheza kutembea kwenda mbele na kurudi nyuma. Wimbo wa *Ndugu yetu* huimbwa kama ifuatavyo:

19. *Ndugu yetu nyamaza twende tukacheze*
    *Mama anakazi hataki tum'beze*
    *Nikubembeleze oooooooooooo*
    *Nikubembeleze oooooooooooo*

Mantiki ya wimbowa *Ndugu yetu* ni kuwajenga watoto tabia njema ya kuwasaidia wazazi kulea watoto.  Aidha, wimbo huu unamuelekeza mtoto mkubwa kumbeba mdogo wake wakati mama anakuwa anafanya kazi za ndani ili mama apate nafasi ya kufanya majukumu yake bila kusumbuliwa na mtoto.Pia wimbo huu, unalenga kuwakuza watoto katika hali ya kuwalinda na kuwabembeleza wadogo zao wanapokuwa wanalia. Hali hii huwakuza watoto katika upendo kwa kupenda baina yao ambapo upendo huo hukua nao mpaka wanapofikia utu uzima.

#### 4.3.1.20 Twende sikukuu

*Twende sikukuu*ni wimbo unaoimbwa katika michezo ya watoto shuleni na hata wakawa wanacheza mtaani au nyumbani. Watoto wenye umri wa miaka 4 hadi 9 hukaa kitako katika kikundi ambapo mmoja huanza kuimba wimbo na wengine wakawa wanaitikia. Wimbo wa *Twende sikukuu* huimbwa kama ifuatavyo:

*20. Twende sikukuu*
*Tukafurahiii*
*Tukapande juu*
*Katika vigariiii*
*Tukaimbe na tucheze*
*Aaaaaaa cheza aaaaaaaa*

Mantiki ya wimbohuo ni kuwajenga watoto tabia njema ya kupenda michezo na burudani mbalimbali. Pia wimbo huu, unalenga kuwakuza watoto kushereheka katika siku za sikukuu kwa kutembea maeneo mbalimbali yaliyotengwa kwa ajili ya burudani. Hali hii huwakuza watoto katika kujenga ushirikiano katika sherehe za sikukuu kwa kutembea, kucheza na kufurahika pamoja.

Katika sehemu hii mtafiti amebainisha nyimbo za michezo ya watoto, miktadha ya uimbaji na mantiki ya nyimbo hizo. Nyimbo zilizobainishwa ni pamoja na *Duara, Moja mbili tatu, Mpilipili, Panya, Maji ya mto, Nalia*na *A, e, i, o, u.* Nyingine ni *Tuamkapo asubuhi, Kidabwada, Turuke ruke, Unakwenda wapi, Ndege kumi porini, Watoto wazuri*na *Baba kasafiri.* Pia, mtafiti amebainishwa nyimbo kama vile *Kijificho, Mnara wa baba, Kasikazi, Sukari ya Mahonda, Ndugu yetu*na *Twende sikukuu.* Sehemu inayofuata inajadili dhamira za nyimbo hizo za michezo ya watoto.

### 4.3.2 Dhamira za Nyimbo za Michezo ya Watoto

Katika sehemu hii mtafiti anadhamiria kujadili lengo mahususi la pili la utafiti huu ambalo lilikusudia kuchambua dhamira zanyimbo za michezo ya watoto katika jamii ya Wazanzibari. Data za utafiti kuhusu lengo hili zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili ambapo mtafiti aliwahoji wahojiwa mbalimbali. Mtafiti alikusanya data za uwandani kutoka kwa wahojiwa ili kupata majibu ya maswali yaliyolenga kujibu lengo hili kama ifuatavyo:

#### 4.3.2.1 Kuwajenga Watoto Kiakili na Kifikra

Nyimbo za michezo ya watoto ni sanaa yenye uwezo wa kuwajenga watoto kiakili na kuwawezesha kufikiri na kukumbuka mambo mbalimbali kwa urahisi. Nyimbo hizi huwasaidia watoto kudadisi jambo, kulikumbuka na kulitekeleza. Halikadhalika, huwafanya kushika kwa urahisi majaribio mbalimbali kutokana na uwezo wake wa kujifunza kuwa mpana. Hapa tuna maana kwamba, mtoto anajifunza vitu vingi kwani hutumia uwezo na nguvu kidogo katika kujifunza tofauti na atakapofundishwa kwa njia ya kuandika tu. Mfano mzuri wa jinsi nyimbo hizo zinavyoweza kuwajenga watoto kiakili na kifikra unaonekana katika wimbo uitwao *Mabata madogo*:

1. *Turuke turuke turuke ruke*
   *Turuke kama ndege wanavyoruka, turuke ruke*
   *Turuke kama njiwa wanavyoruka turuke*
   *Turuke kama chura wanavyoruka, turuke ruke*

Katika wimbo huo tunaona kwamba unamfundisha mtoto tabia za ndege aina ya njiwa, kuruka kwake na hata kutenda kwake. Pia, wimbo huu unamfundisha mtoto tabia ya chura ya kurukaruka akiwa anatembea. Kwa hivyo, wimbo kama huu unapoimbwa mara kwa mara humkumbusha mtoto tabia za njiwa na mdudu chura

hata bila kuwaona.Wimbo mwingine unaofanana na huu, ambao nao una dhamira ya kuwajenga watoto kiakili na kifikira ni wimbo wa *Watoto wazuri:*

2. *Sisi watoto wazuri, tucheze uwanjani*
   *Tukiondoka uwanjani,tukimbilie nyumbani*
   *Tusicheze barabarani,pamoja na misingini*
   *Tusikubali kuitwa,kupewa pipi na pesa*
   *Njiani kuna vibaka,hatari watatubaka*
   *Hatudanganyiki.*

Katika wimbo huo tunabaini kuwa unalenga kuwakuza kiakili na kifikira. Kupitia wimbo huo watoto hujengeka ujasiri wa kucheza ili wawe wachangamfu kimwili na kiakili wanapokuwa darasani na nyumbani. Pia, wimbo huu una dhamira ya kuwafunza watoto kucheza katika mazingira yaliyo salama kama vile uwanjani na kuwataka wajiepushe kucheza katika maeneo hatarishi kama vile barabarani na kwenye mitaro. Pia, wimbo huo unadhamira kuwajenga tabia njema watoto ya kutokubali kuitwa na kupokea zawadi kutoka kwa watu wasiowajua wanapokuwa katika michezo au wakiwa njia. Hii ni kwa sababu dunia imebadilika, baadhi ya watu hawana nia njema kwa watoto hao kiasi kwamba wanapokubali kupokea zawadi kutoka kwao wanaweza kutumia nafasi hiyo kuwafanyia vitendo vya udhalilishaji.

Aidha, dhamira ya kuwajenga watoto kiakili na kuwakuza kifikira tunaiona kupitia wimbo wa *Ndege kumi:*

3. *Ndege kumi porini juu ya mti wamelala*
   *Wamelalia furaha, furaha ya maisha*
   *Wakwanza ameruka*
   *Wapili akaruka*
   *Watatu akaruka*

*Wanne akaruka*
*Watano akaruka*
*Wote wameruka wote wameruka*
*Wameruka juu kabisa*

Katika wimbo huo tunabaini kuwa unawajenga watoto tabia ya kufanya mazoezi ya kuchangamsha mwili ili wawe wachangamfu kiakili na kifikira wanapokuwa darasani. Tunapouchunguza kwa makini wimbo huo huambatana na vitendo vya kurukaruka ambavyo humfanya mtoto achangamke. Pia, ndani yake unawajenga watoto hao katika stadi za kuzungumza, kusikiliza na kuhesabu. Hivyo basi wimbo huu, huwakuza watoto katika hali ya uimara na uchangamfu.

Maelezo kuwa nyimbo za michezo ya watoto huwajenga kiakili na kifikira yanaungwa mkono na Bakize (2014). Bakize anaeleza kuwa nyimbo za michezo ya watoto ni nyenzo muhimu katika kuwakuza kiakili na kifikira watoto. Anaendelea kueleza kuwa nyimbo za michezo ya watoto mara nyingi huwa na maelezo ya kufurahisha, hadithi za kusisimua na ubunifu. Katika kusikiliza na kushiriki kuimba nyimbo hizo, watoto wanaweza kujifunza kufikiria na kutumia mawazo yao kujenga maoni na mawazo mapya. Aidha, nyimbo hizo zinaweza kusaidia katika kuendeleza uwezo wa watoto kusikiliza na kufuatilia ambao ni ujuzi muhimu katika ukuaji wa kiakili na kifikira.

Kwa kuzingatia maelezo hayo, ni wazi kwamba nyimbo za michezo ya watoto ni muhimu katika kukuza ukuaji wa kiakili na kifikira kwa watoto.Kwa sababu nyimbo husaidia kuchochea ubunifu wa mawazo, kuendeleza uwezo wa kusikiliza na kufuatilia na kuimarisha kumbukumbu za mambo mbalimbali.

#### 4.3.2.2 Kuwafunza na Kuwaendeleza Watoto Kimaadili

Nyimbo za michezo ya watoto huwafundisha watoto na kuwajenga maadili na tabia njema zinazokubalika katika jamii. Miongoni mwa mambo ya kimaadili ambayo mtoto huweza kujifunza kupitia nyimbo ni heshima kwa wakubwa, kusema asante apewapo kitu chochote, kutoharibu vitu na maadili juu ya kuthamini vitu na viumbe ambavyo ni hazina kwa jamii. Wimbo ufuatao unaonesha umuhimu wa mtoto kusalimia wazazi na wakubwa wake:

4. *Tuamkapo asubuhi*
   *Tuwasalimie wazazi*
   *Shikamoo baba shikamoo mama*
   *Hiyo ndio tabia njema*

Katika wimbo huo tunabaini kuwa unadhamiria kuwajenga watoto kuwa na tabia njema ya kuwasalimia wazazi wao kila waamkapo asubuhi. Pia, wimbo huo unawaonesha watoto umuhimu wa tabia ya kuwasalimia wazazi pamoja na watu wengine kila wanapoamka au wanapokutana nao kwa siku. Kwa muktadha huo, wimbo huu una dhamira ya kuwakuza watoto katika hali ya heshima na adabu njema katika jamii yao. Watoto waliokuzwa katika hali ya heshima na adabu huwa na maadili mema ambapo hujiepusha na vitendo viovu vinavyochangia mmongonyoko wa maadili katika jamii.

Wimbo mwingine ambao una dhamira ya kumjenga mtoto katika tabia njema ya maadili na heshima ni wimbo wa *Mpilipili*. Kupitia wimbo huu mtoto anajengwa kuwaheshimu wageni wanapokuja nyumbani: Tuchunguze wimbo wenyewe:

5. *Mpilipili mti gani wa kuinama inama aaaa*
   *Inama mimi nasema na wewe wanishikia matama aaaaa*

*Inama mgeni akija eee*
*Tumpokee Inama mgeni akija ee Tumpokee Inama*

Katika wimbo huo tunabaini kuwa unadhamiria kuwajenga watoto kuwa na heshima kwa wakubwa zao katika maisha yao ya kila siku. Hivyo basi, watoto wanapaswa kuwa na heshima kwa wageni waliofika nyumbani kwao. Kupitia wimbo huu, watoto hujengwa wawe na tabia ya kuwasalimia wageni kwa heshima ikiwa ni pamoja na kuwalaki wageni waliotembelea nyumbani kwao. Kwa hivyo, tabia ya kuwa na heshima huwasaidia watoto kukua katika malezi na maadili mema ambayo hudumu nayo hadi katika maisha ya utu uzima.

#### 4.3.2.3 Kuwaburudisha na Kuwastarehesha Watoto.

Mulokozi (2017) anaeleza kuwa nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa katika jamii za Kiafrika. Anafafanua kwamba nyimbo zinaweza kutumika kuwaburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko. Kupitia maelezo hayo ya Mulokozi, watoto wanapokuwa shuleni, huimba kwa mazoea bila ya kufahamu kuwa wanajiburudisha na kujifunza mambo mbalimbali. Wakati mwingine, nyimbo hizi humshirikisha mtoto na viungo vyake vya mwili wakati wa kuimba na kutenda. Kwa mfano, katika wimbo wa *Kidabwada:*

6. *Kidabwada mkia kamata*
   *Kamata kichwa kamata*
   *Kamata mabega kamata*
   *Kamata tumbo kamata*
   *Cheza chakacha chakacha chakacha*

Kupitia wimbo huo tunabaini kuwa unadhamiria kuwajenga watoto tabia ya kufanya mazoezi ya viungo ili waweze kuwa imara kimwili na kiakili. Hii ni kwa sababu

wimbo huo huambatana na vitendo kama vile kukamata kichwa, mabega na tumbo huku akiwa anacheza. Vitendo hivyo humfanya mtoto achangamke mwili kwani hucheza hadi akawa analoa jasho. Kwa kufanya hivyo mtoto huchangamshwa na kuburudishwa. Katika muktadha huo, wimbo huu unakusudia kuwakuza watoto katika hali ya uchangamfu kimwili na kiakili. Hali ambayo huwajenga afya njema kuwa imara katika shughuli zao za kila siku za maisha.

Aidha,dhamira ya kuwaburudisha na kuwastarehesha watoto tunaibaini katika wimbo wa *Twende sikukuu* kama ifuatavyo:

*7. Twende sikukuu*
*Tukafurahiii*
*Tukapande juu*
*Katika vigariiii*
*Tukaimbe na tucheze*
*Aaaaaaa cheza aaaaaaaa*

Kupitia wimbohuotunabaini kuwa unadhamiriakuwajenga watoto tabia njema ya kupenda michezo na kupata burudani mbalimbali. Vilevile, wimbo huu unalenga kuwakuza watoto kuwa na tabia ya kushereheka katika siku za sikukuu kwa kutembea maeneo mbalimbali ya burudani. Kufanya hivyo, huwakuza watoto kujenga njema ya kuwa na ushirikiano katika sherehe za sikukuu kwa kutembea, kushereheka na kuburudika pamoja.

#### 4.3.2.4 Kuwajengea Watoto Moyo wa Uzalendo

Jukumu jingine la nyimbo za watoto ni kuwajengea watoto moyo wa uzalendo. Pindi mtoto aimbapo nyimbo za kuhamasisha dhamira fulani ni wazi kuwa atajifunza

dhamira hiyo. Kupitia nyimbo mbalimbali, watoto hujifunza dhamira ya uzalendo wa kupenda kitu au nchi yao. Kwa mfano, wimbo *Kasikazi* unabaini kuwa unamjenga mtoto tabia ya uzalendo:

8. *Kasikazi ndio kwetu mie*
   *Kizimkazi sikujui mie*
   *Akitoka baba namuona mie*
   *Mtu wa kazi nyumbani kwetu mie*

Katika wimbo huo tunabaini kuwa dhamira yake nikuwajenga watoto uzalendo wa kupenda makwao badala ya kupenda mahali kwa watu wengine. Aidha, wimbo huu unawajenga watoto moyo wa kupenda kufanya kazi na kuwasaidia wazazi wao kufanya kazi mbalimbali.Wimbo huu pia, unalenga kuwakuza watoto katika hali ya kutunza siri katika siri katika shughuli za maisha yao ya kila. Kwa hakika, kupenda kwenu, kufanya kazi na kutunza siri ni tabia ambayo hupatikana kwa wazalendo.

#### 4.3.2.5 Kuwafunza Matamshi na Kuwajengea Uwezo wa Uvumbuzi

Nyimbo huwafunza watoto kutamka maneno na kumjengea uwezo wa kuvumbua mambo mapya. Katika hoja hii, nyimbo zifundishwazo shuleni zimelenga kumpatia mtoto kujua vitu mbalimbali katika mazingira yake. Kwanza tunaona mtoto anapoziimba hujifunza kutamka na kumfanya awe mwepesi katika kuzungumza, kuongeza misamiati ndani ya ubongo wake na ndipo aanze kuunganisha hiyo misamiati na kuandika. Kwa mfano wimbo wa A, e, i, o, u:

9. *A – Allahuwa Allah*
   *E – Ewe mola wetu*
   *I – Ibariki dua yetu*
   *O – Ombi letu sisi*

*U – Utujaalie*

*Tuwe na afya tuweze kucheza*

Katika wimbo huo, tunabaini watoto wanajengwa ujasiri wa kuwa na uwezo wa kuzitamka na kuzielewa irabu za lugha ya Kiswahili. Pia, kupitia wimbo huo watoto wanajengwa imani ya kuwa maombi yao yote waombe kwa Mwenyezi Mungu mtukufu. Aidha, wimbo huo unaonesha umuhimu wa kuwa na afya njema kwa watoto kwa sababu watoto wanajengwa Imani kuwa ili waweze kucheza ni lazima wawe na afya njema. Hivyo, unalenga kuwakuza watoto katika hali ya tahadhari kwa kuwataka wawe makini katika harakati zao za maisha kila siku ili waweze kuepukana na maradhi ya aina mbalimbali.

Wataalamu wa elimu wanathibitisha kwamba hatua ya kwanza katika kujifunza na kufundisha ni kutamka na kisha kuandika hufuata. Hivyo kwa mtoto kuanza kuimba nyimbo hizi anajifunza sauti mbalimbali za lugha husika na hatimaye hujifunza kuziandika. Kwa muktadha huo, tuliyoyataja hapo juu ni baadhi tu ya dhima za nyimbo za watoto kwa watoto wenyewe na kwa jamii pia. Sehemu inayofuata inajadili dhamira za nyimbo zilivyosaidia kujenga ujasiri na tabia njema.

### 4.3.3 Dhamira za Nyimbo Zinavyosaidia Kujenga Ujasiri na Tabia Njema

Katika sehemu hii mtafiti anajadili lengo mahususi la tatu la utafiti huu ambalo lilinuilia kuchambua dhamira zanyimbo za michezo ya watoto katika jamii ya Wazanzibari. Data za utafiti kuhusu lengo hili zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi ambapo mtafiti aliwafanya mjadala na walimu kuhusu jinsi dhamira za nyimbo zinavyojenga ujasiri na tabia njema. Mtafiti alikusanya data za uwandani kutoka kwa wahojiwa ili kupata majibu ya maswali yaliyolenga kujibu

lengo hilo la tatu. Katika kulifikia lengo hilo, mtafiti kwanza alichunguza jinsi dhamira za nyimbo za michezo ya watotozinavyosaidia kuwajenga ujasiri. Uchambuzi wa data kuhusu kipengele hicho ulikuwa kama ifuatavyo:

#### 4.3.3.1Kuwajenga Ujasiri kwa Kuwakuza Kiakili na Kifikra

Nyimbo za michezo ya watoto ni sanaa yenye uwezo wa kuwajenga watoto kiakili na kuwawezesha kufikiri na kukumbuka mambo mbalimbali kwa urahisi. Nyimbo hizi huwasaidia watoto kudadisi jambo, kulikumbuka na kulitekeleza. Halikadhalika, huwafanya kushika kwa urahisi majaribio mbalimbali kutokana na uwezo wake wa kujifunza kuwa mpana. Hapa tuna maana kwamba, mtoto anajifunza vitu vingi kwani hutumia uwezo na nguvu kidogo katika kujifunza tofauti na atakapofundishwa kwa njia ya kuandika tu. Mfano nyimbo hizo zinavyoweza kuwajenga watoto kiakili na kifikra unaonekana katika wimbo uitwao *Kijificho*:

*10. Kificho ficho*
*Banda jicho*
*Nawe unalo*
*Ilo jicho*
*Kajificheni*
*Fumba macho*
*Ukifumbua shauri yako.*

Wimbo huuu nawajenga watoto ujasiri wa kuwa changamsha ili wakue kiakili na kifikira. Hii ni kwa sababu wimbo huo huambatana na vitendo vya kurukaruka ambavyo humfanya mtoto achangamke. Pia, wimbo huu unalenga kuwakuza watoto katika hali ya uimara wanapokuwa darasani pamoja na kuwajenga watoto hao katika stadi za kuzungumza, kusikiliza na kuhesabu.

#### 4.3.3.2 Kuwajenga Ujasiri kwa Kufanya Kazi kwa Bidii

Utafiti umeonesha kuwa katika nyimbo za michezo ya watoto, kunakusudiwa kuwajenga ujasiri wa kufanyakazi kwa bidii ili kuweza kupambana na hali ya umaskini inayoambatanana njaa. Kupitia nyimbo mbalimbali wanajamii hususan watoto katika familia wanaaswawaache utegemezi kutoka kwa wazazi wao na badala yake wajishughulishe na kazi mbalimbali. Wimbo wa *Kasikazi* unafafanua:

*11. Kasikazi ndio kwetu mie*
*Kizimkazi sikujui mie*
*Akitoka baba namuona mie*
*Mtu wa kazi nyumbani kwetu mie*

Wimbo huo unawajenga watoto moyo wa kupenda kufanya kazi, hususani kazi za uzalishaji pamoja na kuwasaidia wazazi wao kufanya kazi hizo.Wimbo huu pia, unalenga kuwakuza watoto katika hali kupambana katika kufanya kazi za kujipatia kipato na kuendesha maisha yao ya kila.

#### 4.3.3.3Kuwajenga Ujasiri kwa Kuepuka Utegemezi katika Maisha

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa utegemezi ni dhamira nyengine ambayo inajitokeza katikanyimbo za michezo ya watoto ili kuwabidiisha wanajamii wafanye kazi kwa bidii nawaepukane na utegemezi katika maisha. Kwani imeonekana kuwa ndani ya jamiimuna watu wamejigeuza kupe ambapo hutegemea kupata kila kitu kutoka kwawenzao, hali hii inatanabahisha katika nyimbo za michezo ya watoto kuwa si nzurikupitia wimbo ufuatao:

*12. Baba kasafiri baba kasafiri*
*Kasafiri kenda mrima*

*Kila hakumbuka x2*
*Hutaka nijirushe mzima mzima x2*

Kwa mujibu wa wahojiwa wetu, mantiki ya wimbo huu ni kuwajenga watoto tabia njema ya kujua umuhimu wa mzazi kuishi pamoja na familia yake katika maisha ya kila siku. Pia, wimbo huu huwatanabahisha watoto kuwa na tabia ya kufanya kazi iliwasewe tegemezi katika familia. Hii ni kwa sababu mzazi anaposafiri kwenda na mbali watoto wakubwa wanashindwa kufanya kazi za kusaidia familia. Badala yake watoto hao huwa tegemezi katika familia za watu wengine.

#### 4.3.3.4Kuwajenga Ujasiri wa Kutafuta Elimu

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa elimu ni ufunguo wa maisha. Hivyo wazazi ama walezi wanatakiwa wafanye bidii zote katika kuhakikisha mtoto anapata elimu iliyo bora, na sio kumfutika ndani tu akawa anafanya mambo yasiyomuhusu kwasababu bila ya elimu hakuna mafanikio yatakayopatikana duniani na akhera. Pia katika kutafuta elimu, asichaguliwe ni elimu ya aina gani na hatua mbalimbali zichukuliwe kuhakikisha mtoto anapata elimu. Wimbo wa *Baba na mama* unafafanua:

13. *"Baba na mama, msinikataze*
*Kwenda skuli kusoma*
*Elimu ya sasa kama chai moto*
*Ukinywa upulizie*
*a, e, i, o, u………."*

Katika wimbo huo, jamii inatanabahishwa kuwa wasiwanyime watoto fursa ya kupata elimu kwasababuelimu ni nuru ya maisha. Kama tunavyojua elimu ni ufunguo wa maisha ya binadamu, hivyo ni muhimu wazazi kuwapa watoto wao fursa ya kwenda shule kusoma ili wajipatie elimu. Hivyo, kupitia nyimbo za michezo ya watoto wanapata hamasa ya kutafuta elimu na kuwaomba wazazi wasiwazuie kwenda shule kutafuta elimu.

#### 4.3.3.5 Kuwajenga Ujasiri waKupanga Malengo katika Maisha

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa nyimbo za michezo ya watoto zina dhima kubwa katika kuwajenga watoto ujasiri wa kupanga malengo ya maisha yao ya baadaye. Baadhi ya nyimbo za michezo za watoto husisitiza umuhimu wa kuwa na ndoto na malengo makubwa maishani. Kwa kusikiliza nyimbo hizi, watoto wanaweza kuhamasika kuweka malengo yao wenyewe na kufanya kazi ili waweze kuyafikia. Kupitia wimbo wa *Maji ya Mto,* mistari ifuatayo inabainisha:

*14. Maji ya mto yanakwenda*
*Yanakwenda mbele kwa mbele*

Kwa mujibu wa Nadharia ya Mwitikio wa Msomaji, wimbo huo unawahamasisha watoto kujipangia malengo ya maisha yao ya baadaye. Maji ya mto yanakwenda mbele kwa mbele inatafsiriwa kuwa watoto wanatakiwa wapange malengo kwa ajili ya mustakabali wao wa baadaye.

Hoja hii inaenda na maelezo ya Mulokozi (2017) anapoeleza kuwa nyimbo za michezo ya watoto mara nyingi zinaweza kusimulia hadithi za mafanikio na ushindi. Kwa kujifunza kuhusu mafanikio ya wahusika katika nyimbo hizo, watoto wanaweza

kuona mfano wa jinsi malengo yanavyoweza kufikiwa kwa kufanya kazi kwa bidii na kujitolea. Anaendelea kueleza kuwa kupitia nyimbo za michezo ya watoto, watoto wanaweza kujifunza kujiamini na kuthamini uwezo wao wenyewe. Kwa kufanya hivyo, wanaweza kuwa na ujasiri wa kutafuta na kufikia malengo yao ya maisha, hata kama ni magumu.

Maelezo hayo pia yanashadidiwa na Wamitila (2008) anapoeleza kazi za fasihi ya watoto. Wamitila anaeleza kuwa nyimbo za michezo ya watoto zinaweza kuwa chanzo cha hamasa na motisha kwa watoto. Kusikiliza nyimbo zenye ujumbe wa kufurahisha na kusisimua kunaweza kuwafanya watoto wapate nguvu na hamasa ya kufuatilia malengo yao ya baadaye.Baadhi ya nyimbo za michezo za watoto husisitiza umuhimu wa kushirikiana na wenzao katika kufikia malengo. Kwa kushiriki katika nyimbo hizo, watoto wanaweza kujifunza umuhimu wa kusaidiana na kusaidiana katika kutimiza ndoto zao za maisha ya baadaye.

Kwa hiyo, nyimbo za michezo ya watoto zina dhimaya kuwajenga watoto ujasiri wa kupanga malengo ya maisha yao ya baadaye. Hayo hutokea kwa kutoa mifano ya mafanikio, kuhamasisha kujiamini, kuongeza hamasa na motisha na kusisitiza ushirikiano katika kufikia malengo.

### 4.3.4 Kuwajenga Tabia Njema

Katika sehemu hii, mtafiti amewasilisha na kuchambua data zinazoonesha namna nyimbo za michezo ya watoto zinavyowajenga tabia njema. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa nyimbo za michezo ya watoto huwajenga watoto kuwa na maadili mema, kuwa na moyo wa kizalendo na kujiepusha na kiburi. Pia, nyimbo hizo

huwajenga watoto kuwa na tabia ya kufanya mazoezi ya viungo na kuwapenda wazazi. Uchambuzi wa vipengele hivyo ni kama unavyoonekana katika sehemu zifuatazo:

#### 4.3.4.1 KuwajengaTabia ya kuwa na Maadili Mema

Katika utafiti huu pia tumebaini kuwa nyimbo za michezo ya watoto zina dhima za kujenga maadili mema kwa watoto. Baadhi ya nyimbo za michezo za watoto husisitiza umuhimu wa kuwa na moyo wa ukarimu na uvumilivu kwa wenzao. Kwa kufundisha maadili haya kupitia nyimbo, watoto wanaweza kujifunza umuhimu wa kusaidiana na kuonyesha uvumilivu hata katika mazingira magumu. Wimbo wa *Ndugu yetu nyamaza* unabainisha:

*15. Ndugu yetu nyamaza twende tukacheze*
*Mama anakazi hataki tum'beze*
*Nikubembeleze oooooooooooo*

Kwa mujibu wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, wimbo huo unasisitiza watoto kupendana ambapo watoto wakubwa waweze kuwalea wadogo zao. Hivyo, nyimbo za michezo ya watoto huonyesha maadili ya upendo na heshima kwa wazazi, walezi na wengine katika jamii. Kupitia nyimbo hizo, watoto hujifunza umuhimu wa na kupendana katika familia na watu wengine.

Mawazo ya nyimbo za michezo ya watoto kuwajenga tabia ya kuwa na maadili mema yanaungwa mkono na Ameir (1983). Ameir anaeleza kuwa nyimbo za watoto mara nyingi hushughulikia mada za uadilifu na uaminifu. Kwa kushiriki kuimba nyimbo hizo, watoto huelewa umuhimu wa kuwa waaminifu na waadilifu katika

mahusiano yao na katika jamii kwa ujumla.Wanendelea kufafanua kuwa nyimbo za michezo za watoto pia husisitiza umuhimu wa uwajibikaji na kujitolea katika kutekeleza majukumu yao. Kupitia nyimbo hizi, watoto wanapata uelewa wa kufanya kazi kwa bidii na kuwajibika kwa vitendo yao ambayo ni maadili mema katika jamii yao.

Kwa muhutasari, nyimbo za michezo ya watoto ni njia nzuri ya kujenga maadili mema kwa watoto katika jamii husika. Hii ni kwa sababu nyimbo huwasaidia kuelewa, kuishi na kuheshimu maadili ya kijamii kwa njia ya kufurahisha na ya kuelimisha.

#### 4.3.4.2 Kuwajenga Tabia ya kuwa na Moyo wa Uzalendo

Dhima nyingine ya nyimbo za michezo ya watoto ni kuwakuza katika tabia ya uzalendo kwa kuwafundisha watoto kuhusu utamaduni, historia, na maadili ya jamii yao. Wimbo wa *Unakwenda Wapi* unafafanua kama ifuatavyo:

*16. Unakwenda wapi Darisalama*
*Kumsalimu nani Baba na mama*
*Ukikutana nae umpe mkono*

Kwa mujibu wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, wimbo huu unawajenga watoto tabia ya uzalendo wa kuwapenda wazazi, ndugu, jamaa na marafiki katika jamii. Kufanya hivyo ni kuendeleza utamaduni na historia ya jamii husika ambapo hayo ndiyo mambo yanayoonesha uzalendo.

Maoni kwamba nyimbo za michezo ya watoto huwajenga tabia njema ya uzalendo yanakubaliana na maelezo ya Senkoro (1996). Senkoro anaeleza kuwanyimbo za

michezo ya watoto mara nyingi hufundisha kuhusu utamaduni na historia ya jamii fulani. Kwa sababu watoto wanapata ufahamu wa utamaduni wao, kujifunza kuhusu matukio muhimu katika historia ya nchi yao, na kuona umuhimu wa kuendeleza urithi wa kitamaduni. Anaendelea kufafanua kuwa baadhi ya nyimbo za michezo za watoto huhamasisha umoja na mshikamano katika taifa. Kwa kushiriki kuimba nyimbo hizi, watoto wanaweza kufahamu umuhimu wa kuwa na upendo kwa nchi yao na kuona umuhimu wa kuchangia katika maendeleo ya taifa lao.

Katika kuunga mkono hoja hii, Nassor (2016)anaeleza kuwa nyimbo za michezo ya watoto mara nyingi husherehekea vyombo vya kitaifa kama vile bendera, wimbo wa taifa, na viongozi wa kitaifa. Kwa kuimba nyimbo hizi, watoto wanaweza kujifunza kuheshimu na kuthamini vyombo vya kitaifa na kujenga hisia ya kuipenda na kujivunia kwa nchi yao. Aidha, nyimbo za michezo ya watoto mara nyingi huwa na maudhui yanayohusiana na maadili ya kitaifa kama vile uaminifu, uwajibikaji, na kujitolea. Kwa kushirikia na kuimba nyimbo hizo, watoto wanaweza kuelewa umuhimu wa kufuata maadili haya na kuwa raia wema wa nchi yao.

Kwa hivyo, nyimbo za michezo ya watoto zina dhima kubwa katika kukuza tabia ya uzalendo kwa kutoa fursa kwa watoto kujifunza kuhusu utamaduni, historia, na maadili ya jamii yao na kuhamasisha hisia ya upendo na kujivunia kwa nchi yao.

#### 4.3.4.3 Kuwajenga Tabia ya Kuepuka Kiburi na Majivuno

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, nyimbo za michezo ya watoto zina dhima ya kuwajenga tabia ya kuepuka kiburi na majivuno. Kupitia nyimbo hizo, watoto hujifunza kuthamini wengine na kutambua kwamba hakuna haja ya kuonyesha

majivuno ili kuthibitisha thamani yao. Mistari ifuatayo ya wimbo wa *Mpilipili* inafafanua:

*17. Inama mgeni akija eee*
*Tumpokee Inama mgeni akija ee Tumpokee Inama*

Kwa mujibu wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, wimbo huo unamjenga mtoto kuwa na tabia ya unyenyekevu na kuepuka kiburi na majivuno. 'Mgeni akija inama' inaashiria kumuamkia mgeni kwa heshima na unyenyekevu anapofika nyumbani. 'Akija tumpokee' inasisitiza umuhimu wa kumlaki mgeni anapokuja nyumbani ili kuonesha upendo na ushirikiano wa kijamii.

Hoja hii inaungwa mkono na Mazigwa (1991) anapoeleza kuwanyimbo za michezo mara nyingi hufundisha umuhimu wa kushirikiana na wenzao ili kuepuka kiburi na majivuno yanayoweza kuharibu uhusiano na kuzuia ushirikiano wao. Anaendelea kueleza kuwa nyimbo za michezo za watoto hutilia mkazo umuhimu wa kuheshimu wengine na kuonyesha heshima katika mahusiano yao. Kupitia uimbaji wa nyimbo hizo, watoto wanaweza kujifunza kwamba kiburi na majivuno hayana nafasi katika kutenda kwa heshima na upendo.

Aidha, Bakize (2014) anakubaliana na hoja hii kwa kueleza kuwa nyimbo za michezo ya watoto huwajenga tabia ya kujifunza na kukua bila kujali hali yao ya sasa. Kupitia nyimbo hizo, watoto huelewa kwamba kiburi na majivuno vinaweza kuwazuia kufikia mafanikio na maendeleo katika maisha yao. Aidha, nyimbo za michezo ya watoto mara nyingi huwahimiza watoto kujifunza kuhusu hisia zao na kuelewa jinsi wanavyoathiri wengine. Kupitia nyimbo hizo, watoto wanaweza

kufahamu kwamba kujielewa na kuepuka kiburi kunaweza kusaidia katika kujenga mahusiano mazuri na wengine.

Kwa ujumla, nyimbo za michezo ya watoto zinaweza kusaidia katika kuwajenga watoto kuwa na tabia ya kuepuka kiburi na majivuno kwa kufundisha unyenyekevu, kusisitiza umuhimu wa kushirikiana, kuonyesha heshima, kujifunza na kukua, na kujitambua na kujielewa.

#### 4.3.4.4 Kuwajenga Tabia ya Kufanya Mazoezi ya Viungo

Nyimbo za michezo ya watoto huwajenga kuwa na tabia ya kufanya mazoezi ya viungo. Mara nyingi, nyimbo hizo huambatana sauti ya muziki ambayo ni rahisi kucheza kwa watoto. Wakati wa kuimba nyimbo hizo, watoto wanafurahia na kucheza huku wakifanya mazoezi bila kujua. Pia, nyimbo za michezo mara nyingi zinahusisha harakati za mwili kama vile kurukaruka, kukimbia, na kucheza. Kwa kushiriki katika nyimbo hizo, watoto wanahamasishwa kufanya mazoezi ya mwili na kukuza ustadi wa kimwili. Wimbo wa *Turuke ruke* unabainisha:

*18. Turuke turuke Turuke ruke*<br>
*Turuke kama ndege wanavyoruka turuke ruke*<br>
*Turuke kama njiwa wanavyoruka turike*<br>
*Turuke kama chura wanavyoruka Turuke ruke*

Kwa kutumia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, tunabaini kuwa nyimbo za michezo ya watoto hujenga mazingira ya watoto kufanya mazoezi ya kikundi. Kwa kucheza na kurukaruka pamoja na wenzao, watoto wanahamasishwa kushirikiana na kufanya mazoezi kwa furaha na motisha.

Mawazo hayo, yanalingana na Mazigwa (1991) anapoeleza kuwa nyimbo za michezo za watoto zinaweza kusisitiza umuhimu wa kudumisha afya na ustawi wa mwili. Kwa kujifunza na kuimba nyimbo hizo, watoto huelewa umuhimu wa kufanya mazoezi ya viungo kwa afya yao na wanaweza kuhamasika kufanya mazoezi mara kwa mara. Mazigwa anaongezea kuwa nyimbo za michezo ya watoto hutoa fursa ya kipekee kwa wazazi na walezi kushiriki katika mazoezi ya viungo vya mwili pamoja na watoto wao. Kwa kuwa nyimbo hizo zinavutia na kufurahisha, wazazi wanaweza kuhamasika kushiriki na hivyo kuwezesha mazoezi ya kifamilia.

Kwa muhutasari, nyimbo za michezo ya watoto zinaweza kuwa nyenzo bora katika kukuza tabia ya kufanya mazoezi ya viungo kwa watoto. Hii inatokana na nyimbo hizo kutoa fursa ya kujifurahisha, kucheza, kushirikiana, kusisitiza afya na kuhamasisha ushiriki wa familia.

#### 4.3.4.5Kuwajenga Tabia ya Kuwapenda Wazazi

Dhima mojawapo ya nyimbo za watoto ni kuwajenga kuwa na uhusiano mzuri kati ya watoto na wazazi wao. Mara nyingi, nyimbo za watoto huelezea upendo, usalama, na uhusiano mzuri kati ya mtoto na mzazi. Kwa kusikiliza na kushiriki katika nyimbo hizo, watoto wanajenga uhusiano wa karibu na wazazi wao. Wimbo wa *Tuamkapo asubuhi* unabainisha:

*19. Tuamkapo asubuhi*
*Tuwasalimie wazazi*
*Shikamoo baba shikamoo mama*
*Hiyo ndio tabia njema*

Kwa kutumia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji tunabaini kuwa wimbo huo unawashajiisha watoto kuwasalimia baba na mama kila wanapoamka asubuhi kwa sababu kufanya hivyo ndio tabia njema. Aidha, nyimbo za michezo ya watoto hujenga tabia ya uaminifu na kuaminiana, ambayo ni nguzo muhimu katika uhusiano wa mzazi na mtoto. Kwa mfano, nyimbo zinazohusu ahadi za wazazi kwa watoto zinaweza kusaidia kujenga imani na usalama kwa watoto.

Hoja hii inakubaliana na maelezo ya Mulokozi (2017) anapoeleza kuwa kupitia nyimbo, watoto wanaweza kuelezea hisia zao kwa wazazi wao, na wakati mwingine hata kuwasilisha mahitaji yao au wasiwasi walio nao. Nyimbo za watoto sio tu zinawajenga tabia ya kuwasalimia wazazi, bali pia ni njia ya kujenga mawasiliano mazuri kati ya wazazi na watoto, huku wazazi wakijifunza kuelewa hisia za watoto wao. Mulokozi anaendelea kufafanua kuwa nyimbo za watoto mara nyingi huleta furaha na upendo. Kwa kushiriki katika nyimbo hizo, wazazi na watoto hujenga furaha ambazo hujenga uhusiano mzuri na upendo.Hivyo basi, watoto wanaposhiriki katika nyimbo, huwa katika shughuli inayowajenga upendo. Hii inaweza kusababisha hisia za ushirikiano na upendo, kwani wanashiriki katika shughuli inayowafurahisha wote.

Kwa hiyo, nyimbo za watoto dhima kubwa ya kujenga tabia ya upendo kati ya watoto na wazazi wao. Hali hiyo,husaidia jamii kukuza uhusiano wa karibu, kuimarisha mawasiliano, na kuleta furaha na ushirikiano kati ya wazazi na watoto wao katika jamii.

### 4.4 Muhutasari wa Mjadala wa Matokeo ya Utafiti.

Matokeo ya utafiti uliofanyika yanaonehsa kuwa nyimbo za michezo ya watoto, mantiki na miktadha ya uimbaji. Pia, Nyimbo hizo zinaonesha Dhamira za Nyimbo teule za michezo ya watoto. Dhamira hizo ni kuwajenga watoto kiakili na kuwawezesha kufikiri na kukumbuka mambo mbalimbali kwa urahisi. Nyimbo hizi huwasaidia watoto kudadisi jambo, kulikumbuka na kulitekeleza. Halikadhalika, huwafanya kushika kwa urahisi majaribio mbalimbali kutokana na uwezo wake wa kujifunza kuwa mpana. Hapa tuna maana kwamba, mtoto anajifunza vitu vingi kwani hutumia uwezo na nguvu kidogo katika kujifunza tofauti na atakapofundishwa kwa njia ya kuandika tu.  Kuwajenga watoto kiakili na kifikra, Kuwafunza na kuwaendeleza watoto kimaadili kuwaburudisha na kuwastarehesha watoto, Kuwajengea watoto moyo wa uzalendo kuwafunza matamshi na kuwajengea uwezo wa uvumbuzi. Dhamira za nyimbo zinavyosaidia kujenga ujasiri na tabia njema. Kuwajenga ujasiri kwa kuwakuza kiakili na kifikra, kuwajenga ujasiri kwa kufanya kazi kwa bidii, kuwajenga ujasiri kwa kuepuka utegemezi katika maisha, Kuwajenga ujasiri wa kutafuta elimu, Kuwajenga ujasiri wa kupanga malengo katika maisha, Kuwajenga tabia ya kuwa na maadili mema, Kuwajenga tabia ya kuwa na moyo wa uzalendo kuwajenga tabia ya kuepuka kiburi na majivuno, Kuwajenga tabia ya kufanya mazoezi ya viungo na kuwajenga tabia ya kuwapenda wazazi.

### 4.5 Muhutasari

Katika sura hii mtafiti amewasilisha, kuchambua data na kujadili matokeo ya utafiti kuhusu dhamira za nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema katika jamii ya Wazanzibari. Uwasilisha na uchambuzi wa data

umefanywa kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti huu. Aidha, katika surah hii imeoneshwa namna utafiti unavyohusiana na nadharia iliyotumika kuongoza uchambuzi wa data.Mwisho, katika sura hii limetolewa hitimisho la mjadala wa matokeo ya utafiti. Sehemu inayofuata inahusu muhutasari wa utafiti, hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inahusu muhutasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo. Kipengele cha muhutasari kinaeleza kwa ufupi mambo yaliyojadiliwa katika utafiti huu ambayo ni matokeo ya utafiti uliofanyika. Kipengele cha hitimisho kinafunga mjadala wa matokeo ya utafiti na kipengele cha mapendekezo kinapendekeza na kushauri mambo ambayo yanaweza kuchunguzwa zaidi katika tafiti zijazo.

## 5.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza dhamira za nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema katika jamii ya Wazanzibari. Ili kufikia lengo hilo, utafiti uliofanyika uliongozwa na malengo mahususi matatu.Lengo mahususi la kwanza lilikuwa kubainisha nyimbo za michezo ya watoto, mantiki na miktadha ya uimbaji katika jamii ya Wazanzibari. Lengo la pili limeenda kuchambua dhamira za nyimbo teule za michezo ya watoto katika jamii ya Wazanzibari. Lengo la tatu lilikusudia kuonesha jinsi dhamira za nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema.

Kwa minajili ya kufikia malengo mahsusi hayo, utafiti huu ulijielekeza kujibu maswali matatu ya utafiti huu.Mosi, kuna nyimbo zipi za michezo ya watoto, zina maana zipi na zinaimbwa miktadha ipi katika jamii ya Wazanzibari? Pili, ni dhamira zipi za nyimbo teule za michezo ya watoto katika jamii ya Wazanzibari? Na tatu, ni kwa jinsi gani nyimbo za michezo ya watoto husaidia kuwajenga ujasiri na tabia

njema? Maswali hayo yamepata majibu ya kwamba iko michezo mingi tu ya watoto ambayo ndani yake muna nyimbo zenye maana kama ambavyo mtafiti alizibainisha na kuzichambua katikasura ya nne.Kupitia nyimbo hizo jamii inapata kujifunza mambo mengi yakuwajenga ujasiri na tabia. Kwa muhutasari matokeo ya utafiti kuhusu majibu ya maswali hayo ni kama yanavyoonekana katika sehemu zifuatazo:

### 5.2.3 Nyimbo za Michezo ya Watoto, Mantiki na Miktadha ya Uimbaji

Utafiti huu ulibainisha mantiki na miktadha ya uimbaji wa nyimbo za michezo ya watoto. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa kuna nyimbo mbalimbali za michezo ya watoto ambazo zina maana tofauti tofauti na huimbwa katika miktadha mbalimbali. Miongoni mwa nyimbo hizo ni 'Duara', 'Moja mbili tatu', 'Mpilipili', 'Panya', 'Maji ya moto', 'Nalia' na 'A e i o u'. Nyimbo nyingine ni 'Tuamkapo asubuhi', 'Kidabwada', 'Turukeruke', 'Unakwenda wapi', 'Ndege kumi porini' na 'Watoto wazuri'. Aidha, zilibainishwa nyimbo kama vile 'Baba kasafiri', 'Kificho', 'Mnara wa baba', 'Kaskazi', 'Sukari ya Mahonda', 'Ndugu yetu' na 'Twende sikukuu'.

Nyimbo hizo huimbwa katika miktadha mbalimbali ambapo katika kipengele cha miktadha, mtafiti alizingatia umri, jinsia, mahali na wakati. Kwa nyimbo teule ziliimbwa na watoto wa umri kati ya miaka mine (4) hadi tisa (9) ambapo kuna nyimbo huimbwa na watoto wa jinsia zote mbili kwa pamoja na nyingine huimbwa na jinsia moja moja. Vilevile, kwa mujibu wa wahojiwa wetu nyimbo hizo huimbwa katika miktadha ya nyumbani, mitaani na shuleni.Katika muktadha wa shuleni nyimbo hizo huimbwa wakati wa asubuhi na mchana na katika muktadha wa nyumbani na mitaani, huimbwa wakati wa jioni na usiku wa mapema.

### 5.2.2 Dhamira za Nyimbo za Michezo ya Watoto

Utafiti huu ulichunguza dhamira za nyimbo teule za michezo ya watoto. Matokeo ya utafiti yanabainisha kwamba nyimbo za michezo zina dhamira mbali mbali kulingana na mahitaji ya jamii. Miongoni mwa dhamira hizo ni pamoja na kuwajenga watoto kiakili na kifikira, kuwafunda na kuwaendeleza katika maadili mema na kuwaburudisha na kuwastarehesha. Dhamira nyingine ni pamoja na kuwajengea watoto mioyo ya kizalendo, kutafuta elimu, kupanga malengo katika maisha, kuwafundisha kutamka maneno ya lugha, kuwafundisha kuhesabu na kuwajengea uwezo wa uvumbuzi.

Aidha, kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, dhamira za nyimbo za michezo ya watoto hulenga kuwasaidia watoto katika kuwakuza kimwili na kimaadili kulingana na jamii wanayoishi. Hivyo basi, watoto wanaoshiriki kucheza na kuimba nyimbo mbalimbali katika jamii zao, hujenga ujasiri na kuwa na tabia njema kutokana na mafunzo wanayopata kutoka katika nyimbo wanazoimba wakiwa michezoni mwao.

### 5.2.3 Nyimbo za Michezo ya Watoto Zinavyowajenga Ujasiri na Tabia Njema

Utafiti huu ulishughulikia jinsi nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema. Kuhusu kipengele hiki, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba michezo ya watoto inawajenga ujasiri na tabia njema. Kwa upande wa ujasiri, michezo hiyo huwakuza kiakili na kifikra, kufanyakazi kwa bidii, kuepuka utegemezi katika maisha, kutafuta kutafuta elimu na kupanga malengo katika maisha yao ya kila siku.

Ama kuhusu kuwajenga watoto katika tabia njema, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa michezo huwakuza watoto kuwa na maadili mema, kuwa na moyo wa kizalendo, kuepuka kiburi, kufanya mazoezi ya viungo na kuwapenda wazazi. Kwa hakika dhamira hizo, huwajenga watoto kuwa na tabia njema katika jamii ambapo hufanya mambo yanayokubalika na kuacha mambo yote yasiyokubalika katika jamii yao.

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulichunguza dhamira za nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema katika jamii ya Wazanzibari. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba dhamira za michezo ya watoto zina umuhimu mkubwa katika kuwakuza watoto hao kimwili na kimaadili ili wawe raia wema wa sasa na baadaye.Kwa kuhitimisha, utafiti huu unaibua hisia na ari za wazazi wa jamii ya Wazanzibari kuona kuwa umuhimu wa kuwatengea watoto muda maalumu wao wa kucheza michezo mbalimbali ya jadi ambayo ndani huimba nyimbo zenye kutoa elimu kwa watoto na jamii kwa ujumla. Aidha, kupitia utafiti huu mtafiti anaamini kwamba jamii itakuwa tayari kubadilika kutokana na makosa waliyokuwa wanayatenda ama kwa makusudi au bila ya kukusudia ya kuwashughulisha watoto kiasi kwamba wanakosa muda wa kucheza pamoja wanapokuwa mitaani au shuleni. Hata hivyo, kupitia utafiti huu, wizara ya elimu kupitia wakuu washule mbalimbali itakuwa tayari kusimamia michezo ya watoto shuleni. Aidha, itakuwa tayari kushajiisha, kuimarisha na kuendeleza vipindi vya michezo ili kuona watoto wanacheza mashuleni, hususan watoto wenye umri kuanzia miaka 4 hadi 14.

## 5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Nyimbo za michezo ya watoto ni chuo muhimu katika kuwakukuza watoto kimwili na kuwajenga kimaadili. Wakati umefika sasa kwa jamii kuzitambua nyimbo za michezo ya watoto kwa ajili ya kuziimarisha kimatumizi ili ziendelee kudumu kama sehemu ya kusaidia kuwajenga watoto wawe na ujasiri na tabia njema kulingana na maadili ya jamii inayohusika. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, utafiti huu umebaini kuwa nyimbo za michezo ya watoto zimeathiriwa kwa kiasi kikubwa sana na maendeleo ya sayansi na teknolojia kupitia utandawazi. Kwa kuthibitisha hilo, wakati wa ukusanyaji wa data za uwandani, mtafiti alikabiliwa na ugumu wa kuwapata watoto wakicheza na kuimba mitaani katika baadhi ya maeneo ya Shehia ya Mahonda. Hivyo, mtafiti alilazimika kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha watoto wamekusanyika kwa ajili ya michezo na kuimba. Kwa muktadha huo, mtafiti aliwatumia watoto walio shule kucheza na kuimba nyimbo mbalimbali zinaimbwa mitaani nyakati za jioni na usiku.

Aidha, kupitia utafiti huu mtafiti amebaini kuwa baadhi ya michezo imeanza kusahaulika mitaani. Matokeo yake yanasababisha kupotea kidogo kidogo kwa michezo na nyimbo zake katika jamii. Kwa mfano, nyimbo kama vile “Nalia”, “Kidabwada”, “Unakwenda wapi” na “Mnara wa baba” ziliimbwa watoto wachache katika baadhi ya maeneo. Hali hiyo inamaanisha kwamba baadhi ya nyimbo zimeanza kusaulika na zinapotea kidogo kidogo. Pia,baadhi ya watoto hawana mazoea ya kucheza na kuimba na watoto wenzao wakiwa mitaani badala yake watoto hao hubakia majumbani mwao wakitazama runinga au video. Kutokana na matatizo hayo yaliyoibuka, mtafiti anapendekeza kuwa jamii inapaswa kukaa na

kutafakari umuhimu wa nyimbo za michezo ya watoto katika kuwajenga kimaadili ikiwemo ujasiri na tabia njema. Hivyo basi, hatua za makusudi zichukuliwe ili kurudisha utamaduni huu wa watoto kucheza na kuimba pamoja wakiwa mitaani nyakati za jioni. Aidha, mtafiti anapendekeza utafiti mwingine kama huu ufanyike kuchunguza athari za kupuuzwa michezo na nyimbo zake katika jamii. Vipengele vingi vya nyimbo za michezo ya watoto havijaandikiwa na baadhi ya nyimbo hazijabainishwa kwa hivyo ni muhimu kufanyiwa utafiti kwa lengo la kuzihifadhi nyimbo hizo katika maandishi.

Halikadhalika, utafiti kama huu wa athari za mwingiliano wa tamaduni kupitia nyimbo za michezo ya watoto wa jamii anwai kupitia michezo inayorushwa katika vituo mbalimbali vya runinga vya ndani na nje ya nchi.Vilevile, kwa kuwa utafiti huu umebaini kwamba kuna kufanana na kutofautiana kiuimbaji kwa baadhi ya nyimbo katika baadhi ya maeneo, ni vyema utafiti mwingine ufanyike ili kuona iwapo nyimbo hizo zinafanana na kutofautiana dhamira zake.

**MAREJELEO**

Ameir, A. (1983). *Fasihi Simulizi.* Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. Dar-esSalaam: Tanzania Publishing House.

Andanenga, A. A. S. (2002). *Bahari ya Elimu ya Ushairi.* Ndanda: Benedictine Publications.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

L.H. Bakize, (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto,*Dar es Salaam

Balisidiya, M. (1979). *Utafiti, Mbinu za Ukusanyaji Fasihi Simulizi na Hatma yake Lugha yetu*. Dar es Salaam: BAKITA.

Beja, S. K. (2001). *Giriama funeral songs: a functional aesthrtic study* (Doctoral dissertation, University of Nairobi)

Culler, J. D. (1982). *On Deconcentration Theories and Critisms after Structuralism*. New York: Comel University Press.

Finnegan, R. (1970). *Oral literature in Africa.* Nairobi: Oxford University Press.

Haji, A. (1992). *Uhakiki wa Fasihi Kidato cha Kwanza Zanzibar*. Zanzibar: E.W.W Mbweni.

Haji, J. A. (1983). *Fasihi Simulizi.* Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. Dar-esSalaam: Tanzania Publishing House.

Hamad, A. (2008). *Matumizi ya Ushairi na Muziki wa Kiswahili katika Maisha ya kila siku Pwani ya Afirka ya Mashariki*. Zanzibar: BAKIZA.

Hussein, E. (1970). *Alikiona,* Nairobi, Dar: es: Salaam, Kampala: East African Publishing House.

Kahigi, K. (1975). *Lugha katika vitabu vya Watoto*, Dar es Salaam: Kioo cha Lugha, JUZ NA UK 21-34.

King'ei, J. na Kisovi, S. (2005). *Misingi ya Fasihi Simulizi,* Nairobi: Focus Publications.

Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: Age Intenational Publishers.

Mazigwa, S. A. (1991). *Fasihi ya Kiswahili na Utamaduni*. Nairobi. The Jomo Kenyatta Foundation

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi,* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Msokile, M. C. (1991). *Kunga za Fasihi na Lugha.* Dar es Salaam: Educational Publishers and Distibutors Ltd.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi*, Mulika na. 21 uk 1-21.

Mulokozi, M. (1996a). *Fasihi ya Kiswahili* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. (1996b). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. (2017).*Kitangulizi cha Fasihi.*Kiuta Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mwita, M. B. (2009). *Uhakiki wa Mtindo na Maudhui katika baadhi ya Tamthilia za Penina Mlama.* Dar es Salaam: Mulika JUZ 28 uk 1004-128.

Nkwera, F. M. V. (1990). *Tamrini za Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: TUKI.

Omar, S. (2008). *Fasihi na Jinsi: Mfano kutoka Nyimbo* za watoto Tanzania. Kiswahili Juzu. 71, uk 98-106.

Oriedo, E. (2000). Fani *katika Riwaya za Shaban Robert:* Kusadikika, Utubora Mkulima na Siku ya watunzi wote. Hanningtone.

Othman, S. Y. (2007). *Hullabies, Woman Writing Africa*, Nairobi: The Easten Region the Feminist.

Nassor, R.O. (2016). Mchango wa Nyimbo za Watoto katika Kukuza Maadili ya Jamii ya Wapemba. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Sengo, T.Y (1991). *Tungo za Pwani.* Dar es salaam, TUKI.

Senkero, F. E. M. K (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam. KAUTU.

Senkero, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam. University Press.

Senkoro, F. (2003). *Nadharia na Takihakiki*. Dar es Salaam: DUP

Simiyu, W. F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi kwa Shule, Vyuo na NDAKI, Tanzania,* Mwanza: Serengeti Bookshop Mwanza.

TAKILUKI, (1983). *Fasihi Simulizi Zanzibar.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* New York: University of New York.

Timammy. R (2002). *Mombasa Swahili Women Wedding Songs: A Stylistic Analysis.* Tasnifu ya uzamifu Chuo Kikuu cha Nairobi.

Wafula, R. M na Njogu, K. (2007). *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phonix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kazi ya Fasihi. Istilahi na nadharia*. Nairobi. Focus Publication Ltd.

# VIAMBATISHO

**Maswali ya Mwongozo wa Usaili**

Mimi, **Ali Khamis Juma** ni mwanafunzi wa Uzamili kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti wa kuchunguza dhamira za nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema. Kwa heshima kubwa ninakuomba unisaidie katika utafiti wangu kwa kujibu maswali yafuatayo. Ninakuahidi kwamba taarifa zote utakazozitoa katika utafiti huu zitakuwa ni siri na hazitaoneshwa au kutangazwa kwa mtu au kikundi cha watu wa aina yeyote wasiohusika. Maswali

1. Nina orodha ya nyimbo hapa nakuomba ni kuulize maswali kwa kila nyimbo. Je kwa maoni yako nyimbo hizi zina dhamira gani kwa watoto?

2. Je kila nyimbo miongoni mwa nyimbo hizi inachezwa katika muktadha gani, nani washiriki na nini mantiki ya huo wimbo?

3. Unadhani nyimbo zote za watoto zina faida chanya kwa wote au nyingine zina faida hasi? Kama kuna faida hasi ni zipi hizo faida hasi?

4. Mojawapo ya faida za michezo ya watoto ni kuwajenga ujasiri na tabia njema. Naomba unieleze kwa jinsi gani watoto wanafikia lengo hili?

5. Una maoni gani kuhusu nyimbo za michezo ya watoto? Ziendelezwe au zisitishwe?

**Maswali ya Mwongozo wa Mahojiano**

Mimi, **Ali Khamis Juma** ni mwanafunzi wa Uzamili kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti wa kuchunguza dhamira za nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kuwajenga ujasiri na tabia njema. Kwa heshima kubwa ninakuomba unisaidie katika utafiti wangu kwa kujibu maswali yafuatayo. Ninakuahidi kwamba taarifa zote utakazozitoa katika utafiti huu zitakuwa ni siri na hazitaoneshwa au kutangazwa kwa mtu au kikundi cha watu wa aina yeyote wasiohusika. Maswali

6. Je uliwahi kuimba nyimbo na kucheza wakati ukiwa mtoto? Kama jibu ndiyo, nakuomba uniimbie nyimbo tatu unazozijua zinaimbwa katika michezo ya watoto.

7. Nyimbo hizi zina dhamira gani kwa watoto?

8. Naomba unitajie faida chanya na faida hasi za michezo hii kwa watoto?

9. Mojawapo ya faida za michezo ya watoto ni kuwajenga ujasiri na tabia njema. Naomba unieleze kwa jinsi gani watoto wanafikia lengo hili?

10. Una maoni gani kuhusu nyimbo za michezo ya watoto? Ziendelezwe au zisitishwe?

## NYIMBO ZA KUCHEZEA WATOTO

1. **Duara**

   Duara duara hili ni duara

   Mwenzetu hayupo katika duara

   Tukamtafute tukamkamate

   Kisha tumlete katika duara

   Na dada Aisha aingie kati

   Aoneshe mbwembwe

   Katika duara.

2. **Moja mbili tatu**

   Moja mbili tatu nne tano

   Nilipata samaki mkubwa mno

   Na yule mwenye nguvu

   Kwanini akamuachia

   Kanikata kidole

   Nalia iiii mama nalia iiii

3. **Mpilipili**

   Mpilipili mti gani wa kuinama Inama aaaa

   Inama mimi nasema na wewe wanishikia matama aaaaa

   Inama mgeni akija eee

   Tumpokee Inama mgeni akija ee Tumpokee Inama

4. **Panya**

   Panyawatatu vipofu

   Walikwenda kwa mke wa mkulima

   Wakata mkia kwa kisu kikali parampara parara parara mpara parara

5. **Maji ya mto**

Maji ya mtoyanakwenda
Yanakwenda mbele kwa mbele
Yanarudi nyuma kwa nyuma

6. **Nalia**

Mwenzenu minalia minalia minalia
Walilia kitu gani kitu gani kitu gani
Nalilia sina shoga sina shoga sina shoga
Tafuta shoga ako shoga ako shoga ako
Anacheza na shoga akee kwa raha zake x2

7. **A,e,i,o,u**

A - Allahuwa Allah
E – Ewe mola wetu
I – Ibariki dua yetu
O – Ombi letu sisi
U – Utujaalie
Tuwe na Afya tuweze kucheza

8. **Tuamkapo asubuhi**

Tuamkapo asubuhi
Tuwasalimie wazazi
Shikamoo baba shikamoo mama
Hiyo ndio tabia njema

9. **Kidabwada**

Kidabwada mkia kamata
Kamata kichwa kamata
Kamata mabega kamata
Kamata tumbo kamata
Cheza chakacha chakacha chakacha

**10. Turuke ruke**

Turuke turuke Turuke ruke

Turuke kama ndege wanavyoruka turuke ruke

Turuke kama njiwa wanavyoruka turike

Turuke kama chura wanavyoruka Turuke ruke

**11. Unakwenda wapi**

Unakwenda wapi Darisalama

Kumsalimu nani Baba na mama

Ukikutana nae umpe mkono

Acheche chechei Aaa kidaa

**12. Ndege kumi porini**

Ndege kumi porini Juu ya mti wamelala

Wamelalia furaha Furaha ya maisha

Wakwanza ameruka

Wapili akaruka

Watatu akaruka

Wanne akaruka

Watano akaruka

Wote wameruka wote wameruka

Wameruka juu kabisa

**13. Watoto wazuri**

Sisi watoto wazuri Tucheze uwanjani

Tukiondoka Uwanjani Tukimbilie uwanjani

Tusicheze barabarani Pamoja na misingini

Tusikubali kuitwa Kupewa pipi na pesa

Njiani kuna vibaka Hatari watatubaka

Hatudanganyiki.

**14. Baba kasafiri**

Baba kasafiri Baba kasafiri
Kasafiri kenda mrima
Kila hakumbuka x2
Hutaka nijirushe mzima mzima x2

**15. Kificho**

Kificho ficho
Banda jicho
Nawe unalo
Ilo jicho
Kajificheni
Fumba macho
Ukifumbua Shauri yako.

**16. Mnara wa baba**

Mnara wa baba na mama  Njoo pwani njoo
Mnara wa baba na mama  Njoo pwani njoo

**17. Kasikazi**

Kasikazi ndio kwetu mie
Kizimkazi sikujui mie
Akitoka baba namuona mie
Mtu wa kazi nyumbani kwetu mie
Hunipa zawadi ninyamaze mie
Mmmmmh nanyamaza mie

**18. Sukari ya Mahonda**

Sukari ya Mahonda inashira nyingi
Anaeionja huanza vitimbi
Ukijisahau tumbo litakuwa tumbwi
Huwezi kucheza cheza huwezi kucheza cheza

**19. Ndugu yetu**

Ndugu yetu nyamaza twende tukacheze

Mama anakazi hataki tum’beze

Nikubembeleze oooooooooooo

Nikubembeleze oooooooooooo

**20. Twende sikukuu**

Twende sikukuu

Tukafurahiii

Tukapande juu

Katika vigariiii

Tukaimbe na tucheze

Aaaaaaa cheza aaaaaaaa